
# Mashirikiano kwa ajili ya elimu mjumuisho

Moduli ya

2



## Muongozo wa mwezeshaji

Umetayarishwa kwa ajili ya:
Jumuiya ya MECP-Z na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu
The Norwegian Association of Disabled
Umetayarishwa na:
Enabling Education Network

NAD – The Norwegian Association of Disabled

MADRASA EARLY CHILDHOOD PROGRAMME

EENET

Inclusive Learning Approach

[Ufafanuzi wa picha (picha ya jalada)]: Watu watano wamekusanyika nje chini ya mti, wanne wamekaa juu ya vibao na mmoja amesimama. Watatu ni wanawake na wawili ni wanaume. Wanawake wawili wamevaa hijabu na mwanamme mmoja amevaa kanzu. Wote wanamsikiliza mwanamme aliyesimama ambae anazungumza. Mtu huyo amevaa suti, ana mguu mmoja na anatumia gongo la kutembelea. Kando yake kuna flipchati iliyowekwa kwenye stendi ikiwa na michoro ya watu wawili – mtoto wa kiume na mtoto wa kike wakiwa ndani ya nyumba iliyoezekwa bati. Upande mwengine wa flipchati kuna mwanamke aliyesimama akitoa ishara za lugha ya alama. Wote wawili, mwanamke na mwanamme wamewaelekea watu watano wanaowasikiliza].

Unaruhusiwa kusambaza na kusanifu muongozo huu ili uendane na mazingira uliopo. Hata hivyo unapaswa kutoa utambulisho sahihi, chimbuko la idhini, na uoneshe iwapo kuna mabadiliko uliyoyafanya. Unaweza kufanya hivyo kwa namna yoyote inayokubalika, lakini bila kuonesha kuwa mabadiliko au matumizi hayo yamethibitishwa na taasisi inayohodhi haki ya muongozo huu. Huruhusiwi kutumia muongozo huu kwa lengo la kujinufaisha kibiashara. Iwapo utauhariri muongozo huu, kuurekebisha, au kuongezea kilichoandikwa humu, utapousambaza unapaswa kutumia idhini halisi kama iliotumika kabla ya muongozo kufanyiwa marekebisho. Huruhusiwi kutumia kanuni za kisheria au teknolojia ambayo kisheria itawazuia wengine kufanya chochote katika muongozo huu ambacho idhini ya awali imeruhusu. Kwa taarifa zaidi, rejea kwenye kiungo kifuatacho: https://creativecommons.org/licenses/bync-sa/4.0/legalcode

Miongozo hii inapatikana chini ya Leseni ya Creative Commons Non-Commercial 4.0 International

# Yaliyomo

Utangulizi ........................................................................................................ 4
Somo la 1: Kamati za elimu mjumuisho za skuli ............................................. 6
Somo la 2: Jinsi gani kamati ya elimu mjumuisho ya skuli inasaidia skuli kuwa jumuishi zaidi? ......................................................................................... 19
Somo la 3: Kuelewa mahusiano ya kimadaraka /madaraka ............................ 25
Some la 4: Kushirikiana na kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ...................... 34
Somo la 5: Jukumu la Mratibu wa elimu mjumuisho ya skuli ........................... 38
Somo la 6: Fursa za ushirikiano katika jamii zetu ............................................ 46

Vielelezo na vitini

Kielelezo 1.2: Skuli ya msingi na sekondari ya Shungu, Zambia: Tafakuri kuhusu skuli jumuishi na jukumu la Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli .................... 58
Kielelezo 1.3a Visa mafunzo – nini maana ya kamati za elimu mjumuisho za skuli? ............................................................................................................... 63
Kitini 1.3b: Muhutasari kuhusu maana ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ........................................................................................................................ 64
Kitini 1.4a: Simulizi ya Yussuf – muhutasari.................................................... 65
Kitini 1.4b: Simulizi kamili ya Yussuf ............................................................... 67
Kitini 1.4c: Mkabala wa mbinu pacha .............................................................. 70
Kielelezo 3.2a: Kuhaulisha mahusiano ya madaraka/madaraka ....................... 71
Kitini 3.2b: Kufahamu mahusiano ya kimadaraka/madaraka ........................... 74
Kielelezo 5.2: Nakala ya video: Bibi Marvellous Mubi, akitafakari jukumu lake kama Mratibu wa Elimu Mjumuisho, Skuli ya Shungu, Zambia ........................ 76
Kitini 5.3: Shughuli anazoweza kushiriki mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli ........................................................................................................................ 78
Kielelezo 6.1: Picha za jamii ............................................................................ 80
Kielelezo 6.2 Taswira pana ya jamii ................................................................. 83
Kielelezo cha 6.2: Visa vya igizo-dhima ........................................................... 85

# Utangulizi

Lengo la moduli hii ni kuzisaidia jumuiya za watu wenye ulemavu (JWWU) na wanachama wao kutafakari ni nani wanahitaji kushirikiana nae ili kujenga skuli ambazo ni jumuishi katika jamii zao. Hii ikiwemo kuzingatia ni nani JWWU zinahitaji kumkabili, na kuzisaidia skuli kuunda na kuzisimamia kamati za elimu mjumuisho za skuli (SIT). Kitabu hiki pia kimezingatia jinsi ya kutambua rasilimali muhimu na uwezo uliopo katika jamii zao na kuzitumia rasilimali hizo kujenga mtandao imara utakaosaidia elimu mjumuisho

Kama ilivyo kwa Moduli ya 1 (au moduli ya msingi): 'Utangulizi wa Elimu Mjumuisho kwa JWWU', moduli hii inatoa mkazo mahususi wa ujumuishi kwa wanafunzi wote, ikiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu na/au ulemavu, ambao mara nyingi hunyimwa fursa mbalimbali na hutengwa zaidi. Mawazo ya kuongeza ufahamu juu ya elimu mjumuisho katika ngazi ya skuli na ya jamii yanapendekezwa. Katika moduli hii kuna muongozo wa kuiga na kurekebisha mafunzo haya ili kuwezesha kubadilishana ujuzi kuhusu elimu mjumuisho katika ngazi ya skuli na jamii.

Moduli hii pia inatanguliza wazo la wataalamu wa elimu mjumuisho, kwa njia ya waratibu wa elimu mjumuisho wa skuli na wengine, wanaofanya kazi kwa karibu na SIT. Sehemu ya jukumu la Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli ni kuanzisha na kuhimiza ushirikiano kwa ajili ya kujumuisha - kuimarisha ushirikiano kati ya skuli, wanafunzi, wazazi/walezi, jamii na wataalamu wengine; shughuli katika moduli hii zitatoa fursa za majadiliano na kubadilishana mawazo kuhusu mada hii.

Wawezeshaji wanapaswa kutambua kwamba ingawa moduli hii imekusudiwa kuzishauri JWWU kuhusu Kamati za elimu mjumuisho za skuli (SITs), moduli hii haipendekezi njia moja tu ya kuanzisha, kudhibiti na kujihusisha na SITs. Kila skuli inahitaji mratibu wa elimu mjumuisho na SIT ambayo ni rahisi kunyumbulika na kufanyakazi kwa mujibu wa mazingira yao ya kipekee, matatizo na fursa - kwa hivyo hakuna fomula maalum ambayo washiriki wanaweza kufundishwa katika utekelezaji wa majukumu ya SIT. Vivyo hivyo, hakuna taratibu zilizoamuliwa mapema ambazo lazima zifuatwe. Kwa kutoa baadhi ya taarifa za kimsingi na mifano, moduli hii itawawezesha walimu, waelimishaji na wadau wengine wenye nia ya kubuni mawazo ili kuendana na skuli zao wenyewe. Pia moduli hii itawawezesha kuanza kufanya kazi pamoja kama SIT, kuelekea lengo moja.

## Muda wa mafunzo

Wawezeshaji wanapaswa kurekebisha mafunzo haya ili kuendana na mazingira ya mahali hapo na muda unaopatikana kwao kwa ajili ya mafunzo. Wawezeshaji wanaweza kuamua kutotumia shughuli zote, au kufupisha baadhi ya shughuli ikiwa muda ni mdogo, au kupanua shughuli ikiwa washiriki wanahitaji usaidizi zaidi wa kuelewa mada fulani.

Ikiwa shughuli zote zitatumika, bila marekebisho makubwa, kufupisha au kurefushwa, moduli hii inahitaji takriban saa 18 za mafunzo na itakuwa vyema zaidi ikifundishwa kwa siku 3.

# Somo la 1: Kamati za elimu mjumuisho za skuli

**Ujumbe mkuu**

Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli (SIT) inahusisha kikundi cha watu wanaojitolea ambao wana lengo la kuimarisha sekta ya elimu au kuimarisha skuli yao na wenye lengo linalowaunganisha pamoja– kuifanya skuli yao iwe jumuishi zaidi.

## Maelezo ya usuli kwa mwezeshaji

**Somo la 1, 2 na 3** yanatambulisha wazo la Kamati za elimu mjumuisho za skuli (SITs) kwa JWWU, maana yake, ni nani anayehusika na jinsi ya kuzisaidia na kuziendeleza . Uundaji na uratibu wa awali wa SIT ni jukumu la skuli na mratibu wa elimu mjumuisho(itatumbulishwa katika somo la tano). Hata hivyo, JWWU zina jukumu muhimu katika kushirikiana na kuisaidia SIT kufanya kazi kwa ufanisi na kuifanya skuli iwe jumuishi zaidi. Kuunda SIT kunahusisha kujenga kujiamini, ujuzi, kujitolea na maarifa, na kutoa usaidizi wa vitendo na mafanikio endelevu ya SIT. Jukumu hili ni la skuli na jamii yote.

Kila skuli inahitaji kamati ya elimu mjumuisho ambayo ni nyumbulifu na inayoshughulikia changamoto na fursa kwa kuzingatia muktadha wa skuli hiyo. Hii ina maana kuwa walimu, wafanyakazi na wadau wa jamii watahitaji kubuni mawazo ili yaendane na skuli yao wenyewe - hakuna fomula maalum ambayo washiriki wanaweza kufundishwa. Vivyo hivyo, hakuna taratibu maalum zilizoandaliwa ambazo lazima zifuatwe. Kwa kutoa baadhi ya taarifa za kimsingi na mifano, masomo haya yatawezesha JWWU na wanajamii kubuni mawazo ya kusaidia skuli zao wenyewe. Pia itawawezesha kuanza kushirikiana na skuli yao, kuelekea katika lengo moja.

## Katika somo hili washiriki:

- Watafafanua ni nini maana ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli na ni nani anayeweza kuwa mjumbe katika kamati hiyo (SIT).
- Watajfunza kutoka Zambia kuhusu uzowefu wa kuunda skuli jumuishi kwa usaidizi wa SIT.
- Watatambulishwa mkabala wa mbinu pacha katika elimu mjumuisho.


## Shughuli ya 1.1: Ni nini kamati ya elimu mjumuisho ya skuli?

1 Dakika 30

### Maelekezo

- Andika swali lifuatalo katika flipchati:
    - **Unadhani kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ni nini na inafanya nini?**
- Mtake kila mshiriki achore picha inayoonesha mawazo yake kuhusu maana ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli na inafanya nini. Wahakikishie washiriki kwamba hili si jaribio au mtihani, ni njia tu ya kupata mawazo yao.
- Waambie kila mshiriki kumgeukia mtu aliyeketi karibu naye na kuelezeana mawazo yao kuhusu michoro yao. Baadaye kila jozi (washirki wawili) wakamilishe sentensi hii:
    - **"Tunafikiri kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ni..."**
- Watake washiriki watoe maoni ya jumla na uandike mambo muhimu kwenye flipuchati. Ikiwa mtu yeyote atawasilisha wazo ambalo kwa hakika **si** sehemu ya jukumu la kamati ya elimu mjumuisho ya skuli (SIT), mwezeshaji alishughulikie hili na kuwaomba washiriki kutafakari kwa nini SIT haitakuwa chombo sahihi kufanya hivyo (k.m., pengine SIT haina mamlaka ya kumwadhibu au kumfukuza kazi mwalimu ambaye alifanya jambo la kibaguzi).
- Onesha slaidi ya PawaPointi yenye picha ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli na uwaombe washiriki kutoa maoni yao kwa ufupi juu ya kile wanachokiona.

**Pawapointi** **Somo la 1: Picha ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli**




Mfano wa mkutano wa SIT katika viwanja vya skuli

[Ufafanuzi wa picha: Kuna watu nane waliokaa nje chini ya mti katika umbo la nusu duara. Wamekaa kwenye viti. Nyuma yao kuna skuli na watoto wanacheza nje ya skuli hiyo. Kuna wanawake watatu katika kikundi cha watu waliokaa, mmoja amevaa hijabu. Kuna mtu mwengine amekaa kwenye kitimwendo na mzee aliyeshika fimbo ya kutembelea. Kuna mtu mwengine katika kikundi ambae anatoa ishara za lugha ya alama. Mwanamke mwengine anazungumza huku akiashiria. Kando yake kuna gongo la kutembelea].

## Shughuli 1.2: Tafakuri kuhusu skuli jumuishi na kamati za elimu mjumuisho za skuli kutoka Zambia

1 Dakika 60

Shughuli hii inawawezesha washiriki kusikia watu waliounganishwa na skuli nchini Zambia wakitafakari juu ya kile kinachofanya skuli yao kuwa jumuishi na jukumu la kamati ya elimu mjumuisho ya skuli (SIT). Pia itawasaidia kujizoesha mbinu ya kuchora mawazo ambayo itakuwa na manufaa kwao wanapokuwa

wanafanya kazi  katika taasisi fulan  na wanahitaji kuchanganua na kufikiria kuhusu masuala mbalimbali.

## Maelekezo

- Andika kwenye flipuchati/onesha maswali yafuatayo kwenye PawaPointi:

  1. **Je, skuli nchini Zambia imekabiliana na vikwazo gani vya ujumuishi?**
  2. **Skuli imefanya nini (kwa msaada wa kamati ya elimu mjumuisho ya skuli) kukabiliana na vikwazo hivi?**
  3. **Nani anahusika katika Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli? Je, wanahusika vipi?**
  4. **Ungewapa mapendekezo gani ili kuimarisha kazi zao?**

**Pawa Pointi** **Somo la 1: Maswali ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli**

- Waambie washiriki kuwa tutatazama sehemu ya mahojiano kutoka Zambia na watu wakielezea maoni yao kuhusu skuli jumuishi na uzowefu wao wa kuanzisha na kuhusika katika kamati za elimu mjumuisho za skuli na kisha kujadili maswali.
- Wagawe washiriki katika vikundi vinne na waambie kwamba kila kikundi kitajadili swali moja. (Pia kila kikundi kinaweza kujadili maswali yote manne kwa pamoja. Baadaye maswali yote yatajadiliwa na washiriki wote kwa ujumla.)
- Wape kila kikundi swali moja na hivyo kila swali litafanyiwa kazi na kikundi angalau kimoja. Wanatakiwa kufikiria swali hili wakati wanaagalia video.
- Chezesha video. Inachukua kiasi dakika 10.

**Kielelezo** **Maelezo ya Zambia: Tafakuri juu ya skuli jumuishi na jukumu la kamati ya elimu mjumuisho ya skuli**

- Badala ya kuandika orodha za majibu, waambie kila kikundi warikodi mawazo yao katika **mfumo wa ramani ya kumbukumbu** - mchoro ambao unaweza kuwa na neno moja au kifungu cha maneno katikati, kisha mawazo, maneno na dhana zinazohusiana na neno hili/ maneno yanaongezwa karibu nayo.

**Ramani za mawazo**

- Ramani ya kumbukumbu inaweza kuendana na upendeleo wa baadhi ya washiriki wanaopendelea zaidi kujifunza kwa mtindo wa kuona , huku pia ikiwafaa wale wanaopendelea kujifunza kupitia majadiliano au kuandika maneno (ona mfano hapa chini).
- Ramani ya kumbukumbu hukuwezesha kuonesha uhusiano kati ya masuala tofauti, watu, matukio, na kadhalika. Rangi tofauti, maumbo, mistari/mishale, n.k, inaweza kutumika kutofautisha aina tofauti za taarifa na miunganisho (k.m., maandishi mekundu yanaweza kuonesha suala hasi huku maandishi ya kijani kibichi yakiwakilisha suala chanya).


- Waoneshe washiriki mfano wa ramani ya kumbukumbu ikiwa hawajawahi kutumia mbinu hii hapo awali. Mifano imeoneshwa hapa chini na kwenye slaidi za PawaPointi, lakini pia unaweza kutumia mifano kutoka katika warsha zilizopita ambazo wameendesha. Sisitiza kwamba hakuna njia sahihi au mbaya ya kuunda ramani ya kumbukumbu, kwa hivyo ni sawa ikiwa kila kikundi kitatoa mchoro tofauti na kikundi chengine.



Washiriki wa Zanzibar wakitayarisha ramani ya kumbukumbu


[Maelezo ya picha: Mchoro wa hapo juu unaonesha wanaume wawili na wanawake watatu wakiwa wamezunguka meza, Mwanamme mmoja anaandika kwenye karatasi iliyopo katikati ya meza.]

## Pawapointi Somo la 1: mifano ya ramani za mawazo




Ramani ya kumbukumbu ililyotayarishwa na washriki wa Zanzibar.

[Maelezo ya picha: Mchoro wa duara katikati ambao umeandikwa 'Kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli'. Maduara mengine 8 yamezunguka duara la kati, lililounganishwa katikati na mistari. Maduara yaliyo karibu yana maneno kama vile 'walimu nawazazi].




Mfano wa ramani ya kumbukumbu iliyochorwa na walimu ambao walikuwa wakififikiria jinsi ya kufanya skuli yao iwe jumuishi Zaidi

[Ufafanuzi wa picha: Ramani ya kumbukumbu, iliyo na kisanduku cha maandishi cha kati kilicho na neno muhimu au kifungu cha maneno, na kisha visanduku vinne vya maandishi vyenye umbo la mstatili ndani yake vina maneno yanayoizunguka, iliyounganishwa kwa mistari na mishale].

- Tumia mojawapo ya mbinu zifuatazo za mrejesho ili kuwataka washiriki watoe mrejesho wa jumla na majadiliano na mwezeshaji afafanue hoja zozote zitakazoleta mkanganyiko. Hoja hizo ziandikwe kwenye flipchati au ubao:
    - Angalia kila swali na watake kila kikundi kilichojadili swali lake wataje nukta zao kuu.
    - Kila kikundi kije mbele na kuwasilisha kazi yao na waelezee nukta zao kuu walizozijadili katika swali lao.
    - Waombe kila kikundi kibandike michoro yao ya ramani zao za kumbukumbu katika kuta za chumba cha mafunzo na kisha mwezeshaji akitake kila kikundi kuelezea nukta zao muhimu.
- Wakati wa mjadala wa jumla, unaweza kurejelea madokezo ya mwezeshaji kwenye ukurasa unaofuata (lakini kumbuka hii sio orodha ya majibu na waruhusu washiriki kutoa majibu).

**Tafakuri kuhusu skuli jumuishi na jukumu la kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ya skuli ya Shungu, Zambia**

1. **Je, skuli ilikabiliwa na vikwazo gani vya ujumuishi?**
    - Vurugu na matumizi ya dawa za kulevya
    - Umbali mrefu wa kuifikia skuli
    - Wanafunzi wanaofanya kazi sokoni
    - Vikwazo vya miundombinu/mazingira
    - Vikwazo vya kimtazamo - watoto wenye ulemavu waliofichwa majumbani na unyanyapaa wanaokumbana nao watoto wenye ulemavu katika jamii.

2. **Je, skuli imefanya nini (kwa usaidizi wa kamati ya elimu mjumuisho ya skuli)kukabiliana na vikwazo hivi?**
    - Ilifanya kazi na wanajamii ikijumuisha misikiti, makanisa, soko, zahanati ya afya na polisi
    - iliendesha kampeni za uhamasishaji - kubandika mabango katika jamii yanayohimiza wazazi kupeleka watoto wao shule - hasa wazazi wa wanafunzi wenye ulemavu na wanafunzi ambao wametoroka.
    - Ilifanya kazi kwa karibu na wazazi na walezi
    - Ilirekebisha mazingira ya skuli: njia, ngazi mtelezo, taa katika jengo la skuli na katika vyoo.
    - Ilitoa baiskeli kwa wanafunzi ambao wanaishi mbali na skuli.
    - Ilianzisha bustani jumuishi ya skuli. Wanafunzi kutoka familia maskini sana wanaofanya kazi kwenye bustani hawalazimiki kulipa ada ya skuli

3. **Ni nani anatakiwa kushirikishwa katika SIT na anashirikishwa vipi?**
    - Mwalimu mkuu, msaidizi mwalimu mkuu, walimu, wanafunzi,
    - wafanyakazi wa afya, ustawi wa jamii, viongozi wa makanisa na misikiti, wafanyakazi wa jamii, watunga sheria,
    - wazazi wa watoto wenye ulemavu
    - wazazi ambao ni wapakaji rangi, mafundi ujenzi, na mafundi seremala

4. **Ungewapa ushauri gani kuimairisha kazi yao?**
    - *Waache washiriki wabadilishane mawazo wenyewe hapa*

## Shughuli ya 1.3: Visa mafunzo vya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli

[1] Dakika 45

### Maelekezo

- Wagawe washiriki katika vikundi vya watu wanne wanne au watano watano.
- Toa nakala moja ya Kielelezo 1.3a (visa mafunzo vifupi) na umwombe mtu mmoja katika kikundi asome kwa sauti kila kisa mafunzo. Kila kikundi kijadili na kuamua kama kisa hicho kinaelezea kamati ya elimu mjumuisho ya skuli. Wakumbushe kwamba hakuna jibu sahihi kabisa au lisilo sahihi.

**Kielelezo** **Visa mafunzo: kamati za elimu mjumuisho za skuli ni nini?**

- Baada ya vikundi kujadili visa mafunzo vyote, tumia maelezo yafuatayo kuongoza mrejesho katika mjadala wa pamoja kwa washiriki wote:

### Maelezo kuhusu majibu yanaoweza kutolewa, kwa ajili ya kuongoza majadiliano kwa washiriki wote

| Kisa mafunzo A: Je, hii ni kamati ya elimu mjumuisho ya skuli? |
| --- |
| • Ndio - kwa sababu hakuna muongozo maalumu kuhusu wajumbe wa kamati au wakutane mara ngapi, kwa hivyo si lazima kuwa na idadi maalum, kwa mfano, kamati haina mtaalamu maalumu (inawezekana skuli haina mtaalamu wa mbinu za ufundishaji au mwanasaikolojia) au wataalamu kutoka nje, au kwamba wanakutana mara nne tu kwa mwaka<br>• Hapana... kwa sababu kamati inaonekana kushughulika na masuala ya ulemavu tu – na hususani kwa aina maalumu ya wanafunzi kuliko masuala mengine ya kimfumo – bila ya kuzingatia changamoto nyengine za ujumuishwaji (mf., vijijini kunaweza kuwa na changamoto za ufukara, usafiri wa kwenda skuli, n.k.)<br>• Hapana....... kwa sababu hakuna juhudi zilizochukuliwa kuwashirikisha walimu wengine na pia labda hakuna jitihada zozote zilizochukuliwa kukuza uwelewa wao kuhusu elimu mjumuisho. |

**Kisa mafunzo B: Je, hii ni kamati ya elimu mjumuisho ya skuli?**

- Kisa-kwa sababu dhamira ya timu imejikita katika eneo dogo. Inaandaa mipango kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu tu. Haionekani kufanya kazi katika uwanda mpana wa masuala ya ujumuishaji kwa wanafunzi hawa au wanafunzi wengine wanaokabiliwa na vikwazo katika elimu
- Hapana... kwa sababu wajumbe wake wengi ni wataalamu tu, sio walimu wa kawaida, walimu wa elimu mjumuisho na wadau wengine.

**Kisa mafunzo C: Je, hii ni kamati ya elimu mjumuisho ya skuli?**

- Hapana... kwa sababu ingawa kuna uhusishwaji wa wazazi/walezi, lakini sio shirikishi. Wazazi/walezi wanaambiwa tu kinachoendelea, lakini hawaalikwi kushiriki kikamilifu katika harakati jumuishi za skuli (kubaini changamoto na kuzitatua).

**Kisa mafunzo D: Je, ni hii ni kamati ya elimu mjumuisho ya skuli?**

- Ndio - kwa sababu inahusisha wadau mbalimbali, na inashughulikia changamoto mbalimbali za ujumuishaji

- Malizia kwa kuelezea kuhusu kamati ya elimu mjumuisho ya skulu (gawa kitini 1.3b) na waombe washiriki watafakari vipengele ambavyo hawajawahi kuvifikiria.

**Kielelezo** **Muhutasari wa kamati ya elimu mjumuisho ya skuli**

## Shughuli ya 1.4: Mkabala wa mbinu pacha: Simulizi ya Yusuf

1 dakika75

**Ujumbe muhimu**

Juhudi za kuimarisha ujumuishi wa skuli/elimu zinaweza kugawanywa katika njia 2 pana - mambo tunayofanya ili **kubadilisha mfumo**, na mambo tunayofanya ili **kusaidia mahitaji ya mwanafunzi binafsi**. Tunahitaji kufanya kazi kwenye njia zote mbili kwa wakati mmoja, vinginevyo tutaunda suluhisho la sehemu tu.

## Maelekezo


- Watake washiriki kufanyakazi katika vikundi vidogo vidogo (vinaweza kuwa viukundi vile vile vya mwanzo au vyengine).
- Viambie vikundi kuwa utawapa hadithi. Kisha unaweza kuisoma hadithi hiyo **(Kitini 1.4a Simulizi ya Yusuf - muhtasari)** kwa kikundi kizima AU kuwapa hadithi hiyo washiriki wasome wenyewe au mshiriki mmoja katika kikundi awasomee wengine kwa sauti.
- Wape kila kikundi **Kitini 1.4a** (Simulizi ya Yusuf - muhtasari).
- Wape vikundi maagizo yafuatayo (au yaandike kwenye flipuchati):
    - Soma hadithi ya Yusuf na tazama picha.
    - Katika vikundi vyenu, jadili hatua zote ambazo unafikiri zingetokea katika miaka hiyo 2 ili kumwezesha Yusuf hatimaye kwenda skuli.
    - Andika kila wazo katika vikaratasi tofauti vya kubandika.
- Baada ya dakika 10-20, wape vikundi maagizo yafuatayo (onesha slaidi ya PawaPointi):

**PawaPointi** **Somo la 1: Kutafakari Simulizi ya Yusuf**

- Angalia mawazo yako na yagawe katika makundi mawili.
    - Hatua zinazolenga kubadilisha mfumo, au kufanya mabadilko katika skuli nzima au darasa zima.
    - Hatua zinazolenga kutoa **msaada binafsi kwa mtoto mmoja** au watoto mahususi.
- Tafakari maswali haya:
    - Je, una mizania katika kuchukuwa hatua za kimfumo na hatua za usaidizi kwa mtu mmoja mmoja?
    - Ikiwa sivyo, je unaweza kufikiria hatua nyengine zinazoweza kuimarisha mizania ?
    - Ikiwa hukuchukuwa hatua zozote za mabadiliko ya kimfumo na ukafanya usaidizi wa mtu mmoja mmoja tu, matokeo yangekuwa yepi?
    - Ikiwa hukuchukuwa hatua zozote za usaidizi wa mtu mmoja mmoja na ukafanya mabadiliko ya kimfumo tu, matokeo yangekuwa yepi?

- Waambie kila kikundi kitoe maoni yao katika majadiliano ya washiriki wote.
- Onesha mchoro ufuatao katika flipuchati au PawaPointi: (Ikiwa utauchora katika flipuchati, unaweza kuubandika katika ukuta katika chumba cha mafunzo ili uonekane na washiriki muda wote wa mafunzo).

**PawaPointi** **Somo la 1: mkabala wa mbinu pacha (slaidi 6-7)**




- Waambie washiriki kuwa daima wanapaswa kuzifikiria sehemu zote mbili za ujumuishi–kubadilisha mfumo na jamii ili iwe jumuishi zaidi, lakini pia kutoa usaidizi kwa mwanafunzi mmoja mmoja itakapohitajika.
- Waambie washiriki kwamba ni muhimu sana tuchukue mkabala wa mbinu pacha katika utekelezaji wa elimu mjumuisho. Kufanya kazi kwenye upande mmoja pekee kutatufanya kupata suluhisho kwa baadhi tu ya changamoto, na kufaulu kwa kiasi kidogo (kama vile treni inayokimbia kwenye njia moja - itaendelea kusonga mbele kwa muda, kisha itaacha njia [na kusababisha ajali]!)
- Kuwa na uwezo wa kuandaa mikakati ya kielimu ya kuleta mabadiliko makubwa ya kimfumo na kushughulika mahitaji ya mtu mmoja ya usaidizi sio jambo ambalo shirika lolote au idara ya serikali inaweza kufanya peke yake. **Ushirikiano ndio kiini cha mafanikio ya elimu mjumuisho.** Kwa mfano, NGOs za kawaida zinaweza kuwa na uzoefu zaidi katika kusukuma mabadiliko ya kimfumo kama vile mabadiliko ya sera, wakati mashirika mahususi yanayolenga ulemavu yanaweza kuwa katika nafasi nzuri zaidi kushughulikia mahitaji ya mtu binafsi ya usaidizi, kama vile kutoa

urekebishaji au vifaa. Lakini ikiwa watafanya kazi kwa kujitenga, kila shirika litakuwa likitoa suluhisho la sehemu na nafasi ndogo ya kufaulu.

- Gawa nakala ya **Kitini 1.4c: Mkabala wa mbinu pacha katika ujumuishi.**

**Kitni 1.4c** **Mkabala wa mbinu pacha**

**Ikiwa kuna muda zaidi, unaweza kufanya moja kati ya yafuatayo:**

- Wape waone kama mawazo yao juu ya hatua ambazo wangeweza kuchukua zinaoana na yale yaliyomo katika simulizi ya **Yusuf**
- Waimbee waisome kwa dakika chache (au mshiriki mmoja katika kikundi anaweza kuwasomea wengine kwenye kikundi kwa sauti) na kulinganisha mawazo yao na yale ya hadithi.
- Kisha fanya mjadala wa jumla kwa washiriki wote. Zingatia mawazo yoyote yaliyotolewa katika simulizi kamili ya Yusuf ambayo washiriki hawakuzingatia au ambayo wana.
- Unaweza kuwapa washiriki **Kitini 1.4b** wakisome baadae, hata kama hutakuwa na muda wa kusimamia majadiliano kuhusu kitini hicho.

# Somo la 2: Jinsi gani kamati ya elimu mjumuisho ya skuli inasaidia skuli kuwa jumuishi zaidi?

**Ujumbe mkuu**

Wakati wa somo hili washiriki wataunda wazo la jinsi gani kamati ya elimu mjumuisho ya skuli inaweza kuwa muhimu katika muktadha wao wenyewe. Kwa kuelewa jinsi inavyoweza kuwasaidia, na kusaidia kukabiliana na vikwazo mahususi vya elimu mjumuisho vinavyokabiliwa na jamii na skuli zao, wanapaswa kuhamasishwa kusaidia maendeleo na kushirikiana na kamati za elimu mjumuisho za skuli katika skuli za majaribio.

**Katika somo hili washiriki:**

ü watajadili vikwazo mbalimbali vya ujumuishi vilivyopo katika jumii na skuli zao

ü watajadili jinsi SIT inavyoweza kusaidia kushughulikia vizuizi/vikwazo hivyo na faida za kufanya kazi kwa ushirikiano.

## Shughuli 2.1: Ni matatizo gani kamati ya elimu mjumuisho ya skuli inaweza kusaidia kuyatatua?

1 dakika 45

### Maelekezo

**PawaPointi** **Somo la 2: Ni matatizo gani kamati ya elimu mjumuisho ya skuli inaweza kusaidia kuyatatua?**


- Onesha slaidi za PawaPointi 1-7 katika Somo la 2, ukiwakumbusha washiriki maana na lengo la elimu mjumuisho Pamoja na vikwazo vikuu vya elimu mjumuisho.
- Watake washiriki kufanyakazi katika vikundi vidogo vidogo, ni vizuri zaidi ikiwa wataunda vikundi hivyo kwa kukaa pamoja wanaotoka katika jamii moja au wilaya na kujadili maswali yafuatayo (yaandike maelekezo haya katika flipuchati au yaoneshe katika slaidi ya PawaPointi):

- Je, ni aina gani ya matatizo unayokumbana nayo katika jumuiya yako kuhusiana na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote **wanahudhuria** skuli, **wanashiriki** katika mchakato wa kujifunza, na **kufaulu** kwa uwezo wao wote?


- Wahimize washiriki kufikiria juu ya aina mbalimbali za wanafunzi walio katika hatari ya kutengwa - kwa mfano, wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu, wanaozungumza lugha nyengine, wale wanaotoka katika familia maskini sana, wale ambao wana matatizo ya kitabia au kihisia, wale wanaotoka katika jamii ya makabila madogo, wasichana na wavulana, wale wanaopata matatizo ya kiafya, wale ambao wamepoteza mzazi mmoja au wote wawili.
- Wakumbushe washiriki kufikiria kuhusu matatizo kwa kuzingatia mtazamo wa kijamii uliojadiliwa hapo awali (yaani, kwamba tatizo haliko kwa mwanafunzi bali liko katika jamii/mfumo wa elimu). Kama utaona itasaidia onesha slaidi za 8-9 zinazoonesha mifano ya 'mwanafunzi kama tatizo' dhidi ya 'mfumo wa elimu kama tatizo' ili kuwasaidia kuwakumbusha kuzingatia vikwazo katika mfumo.

**PawaPointi** **Ni matatizo gani ambayo kamati ya elimu mjumuisho ya skuli inaweza kusaidia kutatua?**

- Waambie kila kikundi waandike kila kikwazo walichokitambua kwenye karatasi tupu – (kwa mlalo ▭) – hivi vitakuwa 'matofali'.
- Baadae kila kikundi kibandike ‘matofali’ yao kwenye sehemu ya ukuta wa chumba cha mafunzo ili kutengeneza mchoro wa ukuta wa matofali. Kila tofali linawakilisha kikwazo au changamoto inayowazuia wanafunzi kuweza kuhudhuria, au kushiriki, au kufaulu.
- Onesha slaidi ya 10 ya PawaPointi yenye maelekezo ya shughuli na slaidi ya 11 yenye mfano wa ‘ukuta wa matofali’, (tafadhali kumbuka, mfano huu unahusiana na afya sio elimu)
- Waambie washiriki kwamba wanaweza kufanya jambo kama hilo wanaporejea kwenye jumuiya zao, kukusanya uchambuzi kamili wa vikwazo, hasa katika ngazi ya jamii, kwa kushirikiana na wafanyakazi wenzao, wazazi/walezi na watoto wao.




[Ufafanuzi wa picha: Mchoro huu unaonesha sehemu ya ukuta iliyotengenezwa kwa tabaka 7 za matofali ya mstatili. Baadhi ya matofali yana maneno yaliyoandikwa juu yake kuelezea aina za vikwazo au changamoto].




Mfano wa mchoro wa ukuta wa matofali wa Zanzibar

[Maelezo ya picha: Vipande vya karatasi vimebandikwa ukutani. Kila kipande cha karatasi kinaonesha kikwazo kilichoandikwa juu yake. Kwa mfano; “hakuna mafunzo ya kutosha kwa walimu", na 'mtazamo hasi'. Mwanamme amesimama upande wa kulia wa picha hiyo, akibandika karatasi hizo ukutani].

## Kitendo cha 2.2: Ni kwa namna gani Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli inavyoweza Kusaidia Kutatua Vikwazo vya ujumuishaji?

1 dakika 45-60

Kupitia shughuli hii washiriki watafikiri zaidi kuhusu vikwazo vya ujumuishi na michango inayohitajika ili kuvisuluhisha, pamoja na kutafakari jinsi kamati ya elimu mjumuisho ya skuli inavyoweza kufanya hili kuwa la ufanisi zaidi.

### Maelekezo

- Katika vikundi vyao, waombe washiriki kuchagua kati ya 'matofali' (vikwazo) kutoka katika ukuta wao (wanaweza kuzipeleka kwenye kikundi chao kama wakitaka) na wajadili yafuatayo (pia kwenye slaidi ya 12 ya PawaPointi):
    - Je, kikwazo hiki kingeweza kushughulikiwa vipi? Ni hatua gani ya kivitendo inaweza kuchukuliwa?
    - Nani anahitaji kuhusishwa katika kuchagua, kuendeleza na kutekeleza suluhisho? Kila mtu angefanya nini?
    - Je, ni kwa njia gani kazi ya kamati inaweza kutoa mbinu bora zaidi ya kutatua kikwazo hiki kuliko ikiwa mtu mmoja mmoja watajaribu kukitatua peke yao?
- Viambie vikundi vinakili jadweli lifuatalo kwenye flipuchati na kuandika majibu yao kwenye jadweli (pia kwenye slaidi ya 13 ya PawaPointi):

| Kikwazo | Kikwazo hiki kingeweza kutatuliwa vipi? | Nani wanapaswa kuhusishwa na watafanya nini? | Ni kwa vipi kufanyakazi kama timu kutakuwa na ufanisi zaidi kutatua kikwazo hiki kuliko kila mmoja kufanyakazi peke yake? |
|---|---|---|---|
| [elezea kikwazo cha 1] | | | |
| [elezea kikwazo cha 2] | | | |
| [elezea kikwazo cha 3] | | | |

- Waambie washiriki kufikiria kuhusu mambo yanayofanana kati ya majibu yao kwa kila kikwazo (k.m., suluhisho ambalo litasaidia kukabiliana na zaidi ya kikwazo kimoja).
- Katika mjadala wa pamoja waambie kila kikundi kielezee mojawapo ya mifano yao.
- Hatimaye wape mfano kutoka Zambia kwenye PPT ya 14 ikiwa wakati utaruhusu.



Mfano wa jadweli la uchambuzi wa vikwazo kutoka Zanzibar

[Maelezo ya picha: karatasi kubwa iliyobandikwa ukutani, imegawanywa katika vipengele vinne 4 navyo ni 'vikwazo', ' namna gani?', 'nani?', 'nini?'. Majibu yameandikwa chini ya kila kipengele].


Kamati za elimu mjumuisho za skuli husaidia kutafuta na kuwasaidia wanafunzi wasiokwenda skuli au wanaokabiliwa na vikwazo vya ushiriki na ufaulu

[Ufafanuzi wa picha: Wanawake 4 wamekusanyika wakimsaidia mwanafunzi aliyekaa katika kitimwendo nyumbani kwao mwanafunzi huyo].

# Somo la 3: Kuelewa mahusiano ya kimadaraka /madaraka

**Ujumbe muhimu**

'Madaraka/madaraka dhidi' ni mtazamo ambao mara nyingi tunautumia kuonea madaraka. Tunachukulia kwamba iwapo mtu mmoja/kikundi katika uwiano ana madaraka zaidi, waliobaki katika uwiano huo lazima wawe hawana madaraka/madaraka. Tunachukulia kwamba iwapo asiye na madaraka (dhaifu) atapata madaraka mpya, aliye na madaraka zaidi lazima apoteze sehemu ya madaraka zake, kwa sababu kuna kiwango kidogo sana cha madaraka/madaraka ambazo watu wanaweza kushirikiana pamoja!

Kufikia malengo yetu tunahitaji kubadilisha namna ambavyo sisi (na wengine) tunavyoifahamu madaraka. Hii inamaanisha kutafuta namna ya kurahisisha katika kazi zetu uwepo wa 'madaraka ndani ya' na 'madaraka kwa' – na kuifahamu zaidi madaraka kama rasilimali isiyo na mipaka – bali kuna madaraka ya kumtosheleza kila mtu!

## Maelezo ya usuli kwa mwezeshaji:

Kuna mifano tofauti ya mtazamo wa madaraka iliyoelezwa hapo juu nchini Somalia. Kwa mfano, katika Kamati za Uongozi za Skuli walimu wanaweza kuonekana kuwa na madaraka/madaraka zaidi kuliko wanajamii na wazazi. Walimu pia wanaweza kuwa na wasiwasi kuhusu kukabidhi madaraka kwa wazazi na wanajamii jambo ambalo linaweza kuwafanya kupoteza baadhi ya madaraka yao.

Mtazamo huu wa madaraka/madaraka ambayo upande mmoja unaweza kupata tu ikiwa upande mwengine utashindwa hautatusaidia kufikia jamii tofauti na isiyobagua ambamo wanyonge wanaokabiliwa na ukiukwaji wa haki wanakuwa wenye haki waliojengewa uwezo.

Bila shaka katika mtazamo huu wa madaraka, upande ambao unasimama kupoteza hautatusaidia kwa hiari kubadilisha usawa/uwiano wa madaraka!

Kufanya kazi kwa ushirikiano kama sehemu ya kikundi au timu inaweza kuwa vigumu sana isipokuwa **ikiwa kila mwanachama ataaonekana kuwa sawa** na inatambulika kwamba wanachama wote wanaleta madaraka, ujuzi na uzowefu tofauti ambao wote utasaidia katika kufikia elimu mjumuisho. Hii ni sahihi kwa

JWWU na ni sahihi pia wakati wa kuunda na kuiongoza kamati ya elimu mjumuisho ya skuli.

Shughuli mbili zifuatazo zinachunguza dhana ya madaraka na mahusiano ya kimadaraka. Shughuli huwasaidia washiriki kutafakari juu ya umuhimu wa **mahusiano sawa** na **madaraka ya pamoja** wakati wa kufanya kazi kama sehemu ya timu au kikundi. SIT inaweza kuwa na mratibu lakini mtu huyu **hana** madaraka zaidi kuliko mwanachama mwengine yeyote wa kamati hiyo. SIT haiwezi kufanikiwa ikiwa itatumika kama zana ya kutanua madaraka/madaraka ya kibinafsi.

### Katika somo hili washiriki:

- ü Watachunguza wazo la 'madaraka' na ni nani aliye na madaraka/madaraka zaidi au kidogo ndani ya jamii yetu na jumuiya zetu
- ü Wataelewa umuhimu wa mahusiano sawa wakati wa kushirikiana na kufanya kazi kama timu
- ü Wataelewa kwamba 'madaraka dhidi ya' sio njia pekee ya kufafanua madaraka na kwamba 'madaraka na' (madaraka ya pamoja) na 'madaraka ndani ya' (madaraka ya mtu binafsi) ni muhimu kwa ajili ya kuelekea kwenye jamii jumuishi zaidi.

## Shughuli 3.1: Mistari ya madaraka/nguvu

1 dakika 45

### Maelekezo

- Bandika alama mbili kwenye ncha tofauti za chumba: moja inasema 'ana madaraka/nguvu', nyengine 'hana madaraka/nguvu'. Lazima kuwe na nafasi wazi kati ya alama hizo mbili.
- Mpe kila mshiriki kadi inayoweza kuganda (yenye gundi) au vipande vya karatasi vinavyoelezea kazi au hadhi. Tazama mifano katika kisanduku hapa chini.
- Waambie washiriki kwamba lazima wote wajifanye kuwa wanaume. Ni lazima wajipange kando ya 'mstari wa madaraka' kutegemea kama wanafikiri mwanamme mwenye kazi/hadhi hiyo ana madaraka/nguvu au hana madaraka/nguvu. Hii inapaswa kutegemea hali katika jamii yao

wenyewe, sio juu ya kile kinachoweza kuwa bora. Washiriki wanaweza kujadiliana na kuhimizana kubadilisha misimamo yao.

**Mawazo ya mifano ya kazi/hadhi**[1]

- Mwalimu wa darasa la kwanza mwenye uzowefu wa miaka 3
- Mtaalamu wa matamshi
- Mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo mwenge umri wa miaka 6
- Mtaalamu wa tibamaungo
- Jaji
- Mwanasaikolojia
- Muuguzi a skuli
- Mulemavu wa akili mwenge miaka 9
- Dakari wa familia
- Mwanafunzi asiye na ulemavu mwenye miaka 7
- Afisa wa polisi
- Mtu zima mwenge ulemavu anayeisha karibu na skuli
- Mweyekiti was Kijiji
- Mpishi katika skuli
- Ndugu/kaka wa mwanafunzi mwenge ulemavu
- Msaidizi wa mwalimu darasani
- Mhadhiri wa chou kikuu
- Mwalimu wa darasa la 5 mwenge uzowefu wa miaka 25
- Mzazi/mlezi wa mtoto mwenge uleamvu
- Mlinzi wa skuli
- Mwalimu mkuu
- Mwalimu wa michezo
- Dereva wa basi
- Mzazi/mlezi asiye na kazi wa mwananfunzi mwenye ulemavu
- Msafishaji
- Mwalimu wa darasa la 10 mwenye uzowefu wa mwaka mmoja
- Mwanafunzi kiongozi katika sjuli
- Mzazi/mlezi ambaye ni mwanachama wa ‘umoja wa walimu na wazazi’

[1] Mwezeshaji abadilishe kazi hizi ili ziandane na muktadha wa eneo analofanyia mafunzo



Washiriki wakiwa katika shughuli ya mahusiano ya kimadaraka nchini Zamzbia

[Ufafanuzi wa picha: Kiasi washiriki 25 wa kike na kiume wamesimama katika mstari. Kila mmoja amevaa alama mbele ya nguo zao].

- Kisha wape baadhi ya washiriki kikaratasi kinachoonesha kwamba wanapaswa **kujifanya wanawake**. Wape takriban nusu ya jumla ya idadi ya washiriki.
- Washiriki lazima waamue (na wajadiliane) kama wanapaswa kuwa mbele au numa kwenye mstari, kutegemea kama wanafikiri hali yao ya kike inawafanya wawe na madaraka zaidi au kidogo katika jamii yao ya sasa.
- Hatimaye, toa vikaratasi vichache zaidi kwa baadhi ya washiriki, vinavyoelezea **ulemavu au hali nyengine ya afya au utajiri** (k.m., wasioona; wenye ulemavu wa viungo; maskini sana; wanaotoka katika kikundi jamii ya lugha za wachache; mkimbizi; wazee; ana VVU, n.k.). Washiriki lazima watathmini tena na kujadili kama msimamo wao kwenye mstari unahitaji kubadilika. Ufanye mjadala ulenge jinsi jamii inavyochukulia kazi hizi katika hatua hii badala ya kile ambacho SIT au wengine wanapaswa kujaribu kufanya ili kubadilisha hali hiyo.
- Fanya mjadala mfupi wa mjadala washiriki wote kuhusu masuala ya madaraka, ukijadili kwa nini baadhi ya watu wanachukuliwa kuwa wenye madaraka zaidi kuliko wengine, na je, hii inaweza kuwa na matokeo gani katika juhudi za kuifanya elimu kuwa jumuishi zaidi?

## Shughuli 3.2 Michezo ya madaraka

[1] dakika 60

### Maelekezo

- Wagawe washiriki katika vikundi vidogo vidogo na wape maelekezo yafuatayo (waoneshe maelekezo hayo katika PawaPointi):
  - Tayarisha mchezo mfupi–dakika mbili tu.
  - Mchezo uoneshe ‘madaraka/nguvu’
  - Unaweza kuchagua aina ya wahusika wako na namna watakavyoshiriki.
- Baada ya dakika 10 za matayarisho, washiriki waoneshe michezo yao. Kama kuna mud awa kutosha na/au vikundi vingi, mwezeshaji achaguwe baadhi tu ya vikundi kuwasilisha michezo yao.
- Once participants have performed, lead a brief plenary discussion about the plays to draw out some of the key elements; for example: Baada ya washiriki kuonesha michezo yao, mwezeshaji aongoze mjadala mfupi wa Pamoja kuhusu michezo hiyo na aoneshe nukta muhimu zilizojitokeza; kwa mfano:
  - Nani alikuwa na madaraka/nguvu?
  - Nani alikosa madaraka/nguvu?
  - Je, madaraka/nguvu yalioneshwa vipi?
- Waombe washiriki watoe maana ya madaraka/nguvu, na uandike majibu yao katika flipuchati.
- Wasilisha nukta muhimu zifuatazo(na onesha slaidi za PawaPointi 3-5). Jaribu kutoa mifano yako mwenyewe wakati unawasilisha kwa washiriki ili uwasidie kuelewa.

**PawaPointi** **Somo la 3: Kuelewa mahusiano ya kimadaraka**

Kuna vyanzo tofauti vya madaraka au sababu katika maisha zinazowawezesha watu kuwa na madaraka, ambapo sisi kama mtu mmoja mmoja hupata madaraka hii kwa kujua au kutokujua. Kwa mfano:

- Elimu, uzoefu wa kazi, hadhi na mali
- kipaji cha kusikiliza, nafasi katika mamlaka, madaraka ya ushawishi

- kipaji cha uchambuzi, udhibiti juu ya rasilimali, ujuzi wa utatuzi wa migogoro

Madaraka inaweza kuwa ya mtu binafsi au ya kikundi cha watu, kama inavyooneshwa na tafsiri ifuatayo:

> **"Madaraka/Nguvu ni uwezo wa kutekeleza malengo binafsi na kuwashawishi wengine kufikia malengo hayo. Ni uwezo wa kupata tunachokitaka, kuhodhi tulichonacho, na kusawiri matukio katika namna tunayotaka yawe."**
>
> **"Kwa ngazi ya kikundi, madaraka/nguvu ni uwezo wa kuunganisha vyanzo tofauti vya madaraka za mtu mmoja mmoja ili kuleta mabadiliko tunayoyatamani ambyo hunufaisha kikundi badala ya mtu mmoja mmoja."**

- Waambie washiriki kwamba madaraka inaweza kugawanywa kama ifuatavyo (Onesha slaidi ya PawaPointi):
  - **Madaraka zaidi:** falsafa hii inaamini kwamba madaraka ni kitu maalumu – mtu mmoja ama kikundi kinapopata madaraka zaidi, wengine hupunguziwa.
  - **Madaraka kwa:** aina hii ya madaraka inaelezea aina fulani ya **uwezeshaji.** Inamuwezesha mtu kudhibiti au kusimamia hali fulani kwa manufaa yake.
  - **Madaraka na:** hii inajumuisha **madaraka ya pamoja** na huonekana pale kikundi kinapotatua changamoto pamoja, na kutengeneza madaraka ambayo ni kubwa kuliko jumla ya madaraka za watu wanaounda kikundi hicho.
  - **Madaraka ndani ya:** madaraka hii inaishi ndani ya mtu na inawakilisha madaraka ya ndani. Inatokana na **kujikubali na kujiheshimu,** ambayo nayo hutokana na kuwaheshimu wengine na kukubali kwamba watu wote ni sawa.
- Uliza maswali yafuatayo kwa washirki:
  - Ni aina gani ya madaraka mnadhani mchezo wenu ulionesha?
  - Je, kulikuwa na aina moja ya madaraka iliyojitokeza katika michezo yote?

[**Maelezo kwa mwezeshaji:** Kuna uwezekano mkubwa kuwa madaraka dhidi ya/ zaidi ilijitokeza katika michezo mingi]

- Watake washiriki kulinganisha maana zao za madaraka (zilizoandikwa kwenye flipuchati) na zile zinazowasilishwa kwenye slaidi za PawaPointi. Kitu gani kilichofanana na au kilichotofautiana?
- Toa seti ya kadi za picha 3 zinazowakilisha sura 3 za madaraka kwa kila kikundi kidogo. Katika vikundi vyao waambie (onesha maelekezi katika PawaPointi)
    a) Waangalie picha hizo na waamue aina ya madaraka inayooneshwa na kila moja kati ya picha hizo.
    b) Ziweke picha hizo kwa mpangilio na usimulie hadithi inayomo katika picha hizo.
    c) Jadili jinsi hadithi hiyo inavyoonesha mabadiliko ya mahusiano ya kimadaraka

**Kitni 3.2a** **'Picha za adaraka'**

- Baada ya dakika 10 watake washiriki wote kutoa mrejesho kutoka katika vikundi vyao.
- Onesha slaidi inayofuata ya PawaPointi yenye picha zote tatu kwa mpangilio. Tumia madokezo kwenye ukurasa unaofuata ili kuchangia katika mjadala ikihitajika. Vidokezo vinatoa tafsiri moja ya picha hata hivyo, kunaweza kuwa na tafsiri nyengine, kwa hivyo uwe tayari kuzikubali tafsiri hizo ikiwa washiriki watatoa mawazo tofauti.

**Picha ya 1 Madaraka/Madaraka dhidi ya**

Picha hii inamuonesha mwanamke mtanashati, ambaye huenda ni mwalimu mkuu akionekana kama kwamba anakataa kuandikishwa skuli mtoto asiyeona. Mama wa mtoto anazungumza na mwalimu mkuu, inaonekana kama kwamba anamuomba aruhusu mwanawe kuandikishwa katika skuli hiyo lakini hana madaraka ya kumshawishi kwa jinsi hali ilivyo. Fikra ni kwamba mwalimu mkuu ana madaraka dhidi ya mama wa mtoto mwenye ulemavu. Mwalimu mkuu anaweza pia kujihisi ana udhaifu fulani akihisi kwamba skuli yake haina mazingira wezeshi kwa mtoto.

**Picha ya 2: Madaraka na**

Picha hii inamuonesha mama wa mtoto asiyeona akiwa kwenye kikao na kamati ya ujumuishi ya skuli (SIT) kujadili jambo fulani. Anasikilizwa na

wajumbe wa kamati na huwenda anahisi anaungwa mkono na wanaomsikiliza na kwamba hayupo peke yake katika changamoto inayomkabili. Mwanawe pia yupo kwenye kikao. Inaonesha kwamba anajisikia ana madaraka na kamati inayomsikiliza, madaraka ya pamoja kwa kutatua changamoto pamoja.

**Picha ya 3 Madaraka ndani ya**

Picha inamuonesha mama wa mtoto asiyeona akiwa amesimama nje ya skuli anazungumza na wadau mbali mbali wa skuli. Kuna watu wengi waliokaa wakimsikiliza. Mwanawe yupo kando yake, akiwa ameshika mkono wa mtu, anaeonekana kuwa ni baba yake. Uwepo wa baba yake unaonesha kwamba anashirikiana kwa karibu na mkewe. Mwalimu mkuu amejumuika na wajumbe wengine kumsikiliza mama wa mtoto asiyeona. Inaonesha kwamba mama wa mtoto anajisikia kuwa na madaraka ndani yake na hata lugha yake ya ishara ni tofauti na mara ya mwanzo alipokutana peke yake na mwalimu mkuu, anaonekana amewezeshwa na mwenye kujiamini.

- Maliza somo kwa kuelezea nukta muhimu zilizopo hapa chini (na uonesha slaidi za PawaPointi). Zihuishe nukta hizo za zile ‘picha 3 za madaraka’:

**PawaPointi** **Somo la 3: Kuelewa mahusiano ya kimadaraka**

- ‘Madaraka dhidi/ zaidi’ ni mtazamo ambao mara nyingi tunautumia kuonea madaraka.
- Tunachukulia kwamba iwapo mtu mmoja/kikundi katika uwiano ana madaraka zaidi, waliobaki katika uwiano huo lazima wawe hawana madaraka. Tunachukulia kwamba iwapo asiye na madaraka (dhaifu) atapata madaraka mpya, aliye na madaraka zaidi lazima apoteze sehemu ya madaraka zake, kwa sababu kuna kiwango kidogo sana cha madaraka ambazo watu wanaweza kushirikiana pamoja!
- Kuna mifano tofauti ya mtazamo wa madaraka iliyoelezwa hapo juu nchini Somalia. Kwa mfano, katika Kamati za Uongozi za Skuli walimu wanaweza kuonekana kuwa na madaraka/madaraka zaidi kuliko wanajamii na wazazi. Walimu pia wanaweza kuwa na wasiwasi kuhusu kukabidhi madaraka kwa wazazi na wanajamii jambo ambalo linaweza kuwafanya kupoteza baadhi ya madaraka yao.

- Mtazamo huu wa uwiano wa madaraka ambapo upande mmoja unaweza tu kupata madaraka iwapo upande mwengine utapoteza hautotusaidia sisi kufikia lengo la jamii jumuishi na isiyo na ubaguzi.
- Bila shaka katika mtazamo huu wa madaraka, upande ambao unasimama kupoteza hautatusaidia kwa hiari kubadilisha usawa/uwiano wa madaraka!
- Kufikia malengo yetu tunahitaji kubadilisha namna ambavyo sisi (na wengine) tunavyoifahamu madaraka. Hii inamaanisha kutafuta namna ya kurahisisha katika kazi zetu uwepo wa 'madaraka ndani ya' na 'madaraka kwa' – na kuifahamu zaidi madaraka kama rasilimali isiyo na mipaka – bali kuna madaraka ya kumtosheleza kila mtu!
- Waombe washiriki washirikiane katika jozi au vikundi vidogo vidogo, kujadili hali ambazo wamezijua ambazo aina nyengine za madaraka (k.m., madaraka na au madaraka ndani ya) zimezingatiwa.
- Toa nakala za Kitini 3.2b: Kuelewa uhusianio wa madaraka ili washiriki wapate muhutasari wa masuala yaliyojadiliwa

## Kitni 3.2b Kuelewa mahusiano ya kimadaraka

# Some la 4: Kushirikiana na kamati ya elimu mjumuisho ya skuli

### Ujumbe muhimu

Ijapokuwa wewe sio sehemu ya wajumbe wa kamati ya elimu mjumuisho ya skuli (SIT) una jukumu kama mwanachama wa JWWU, mzazi au mwanajamii kusaidia na kushirikiana na SIT ili kuisaidia skuli yako iwe jumuishi zaidi. Jumuiya za Watu wenye Ulemavu (JWWU) zimepata mafunzo ya kina kuhusu elimu mjumuisho ikilinganishwa na wanachama wengi wa SIT. Hivyo basi kubadilishana ujuzi na maarifa na JWWU kuhusu elimu jumuisho ni nini, jinsi inavyotofautiana na elimu maalum na jinsi tunavyoweza kwa pamoja kushughulikia vikwazo vya elimu mjumuisho ni rasilimali kubwa kwa SIT.

## Maelezo ya usuli kwa mwezeshaji

- Ushirikiano unahitajika kati ya wazazi, jamii na skuli ili kuleta maendeleo kuelekea elimu mjumuisho. Hii ni pamoja na kuunda na kuimarisha ushirikiano kati ya skuli, wanafunzi, wazazi/walezi, jamii na wataalamu wengine.
- Wazazi na jamii mara nyingi huwa hawashirikishwi katika sekta ya elimu na inawezekana wakawa hawajui huduma zinazotolewa, na msaada na elimu wanayoweza kuitoa. Walimu wengi na waelimishaji wengine hufanya kazi peke yao na hukabiliana na changamoto katika kukidhi mahitaji ya wanafunzi wote wanaowashughulikia. Wakati mwengine hufanya kazi kwa bidii lakini hukosa uungwaji mkono, fursa za mafunzo na vitendea kazi vya kuwasaidia kuwa jumuishi zaidi.
- Juhudi na hatua za kuzifanya skuli ziwe jumuishi zaidi na kushughulikia vikwazo vya elimu mjumuisho mara nyingi huanzishwa na miradi inayofadhiliwa na wafadhili na wakati ufadhili au mradi huo unapoisha hatua zenyewe pia zinaweza kuisha, kumaanisha kuwa haziwezi kudumu. Hii inaweza pia kuwa kweli kuhusu maendeleo na shughuli za kamati za elimu mjumuisho za skuli. Wakati wa kuanzisha na kusimamia kamati hizi skuli na jamii pana kwa hivyo zinahitaji kuzingatia kile kinachohitajika kuwepo ili kuhakikisha kamati hiyo ni endelevu kadiri iwezekanavyo.

**Katika somo hili washiriki:**

- ü Watajifunza maendeleo ambayo yamepatikana katika uundaji wa kamati za elimu mjumuisho za skuli kwa skuli za majaribio katika wilaya zao
- ü Tafakari jinsi JWWU zinavyoweza kuongeza thamani/kuchangia kwenye kamati za elimu mjumuisho za skuli kwa ufanisi zaidi

## Shughuli 4.1: Kutafakari juu ya uanzishwaji wa kamati za elimu mjumuisho za skuli

Kabla ya shughuli hii, unapaswa kuwauliza wanachama wa JWWU ambao tayari wamejihusisha na SIT kujiandaa kutoa uzowefu wao. Zaidi ya hayo, au vyenginevyo, unaweza kumwalika mwalimu mkuu kutoka skuli ambayo tayari imeanza shughuli na SIT yao kuja na kutoa uzowefu wao.

1 dakika 45

### Maekekezo

**PawaPointi** **Kushirikiana na Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli**

- Wasilisha nukta zifuatazo katika PawaPointi:
  - Wazazi na jamii mara nyingi huwa hawashirikishwi katika sekta ya elimu na inawezekana wakawa hawajui huduma zinazotolewa, na msaada na elimu wanayoweza kuitoa.
  - Walimu wengi na waelimishaji wengine hufanya kazi peke yao na hukabiliana na changamoto katika kukidhi mahitaji ya wanafunzi wote wanaowashughulikia. Wakati mwengine hufanya kazi kwa bidii lakini hukosa uungwaji mkono, fursa za mafunzo na vitendea kazi vya kuwasaidia kuwa jumuishi zaidi
  - Kwa ufupi, mara nyingi kuna **ukosefu wa ushirikiano**, ambao ni lazima uwepo iwapo skuli na jamii inahitaji kuwa jumuishi.
- Kwenye PawaPointi (au flipuchati) onesha muhtasari wa uundaji wa SIT katika skuli za majaribio hadi sasa. Katika ngazi ya wilaya/mtaa muhtasari huu utalenga skuli za majaribio tu zilizo katika wilaya hiyo. Muhtasari huu unapaswa kutegemea kile ambacho kimetajwa katika ripoti za Wakufunzi

wakuu kutoka katika skuli za majaribio. Muhtasari unapaswa kujibu maswali yafuatayo na uandikwe kwenye slaidi ya PawaPointi au flipuchati:

- Ni hatua gani zilizopigwa na skuli za majaribio katika uundaji wa SIT?
- Ni skuli zipi za majaribio ambazo tayari zimeanzisha SIT?
- Nani wanahusishwa katika SIT?
- Ni zipi zimekuwa shughuli zinazofanywa na SIT hadi sasa?

- Karibisha maswali/maoni kutoka kwa washiriki.
- Waulize wanachama wa JWWU ambao tayari wamejishughulisha na SIT watoe uzowefu wao (utahitaji kuwaomba mapema ili wajitayarishe). Katika ngazi ya wilaya/mtaa, waalike walimu wakuu wa skuli za majaribio na/au mwanachama mwengine wa SIT aje kutoa habari kuhusu maendeleo ya SIT yao hadi sasa (hili litahitaji kufanywa mapema).
- Karibisha mjadala na maswali kutoka kwa washriki wengine katika chumba cha mkutano.

## Shughuli 4.2 Ushirikiano wa JWWU na SIT.

1 dakika 75

### Maelekezo

**PawaPointi** **Kushirikiana na SIT**

- Onesha slaidi 3 ya PawaPointi. Wakumbushe washiriki kwamba hata kama wewe si sehemu moja kwa moja ya SIT kama mwanachama, una wajibu pia kama mwanachama wa JWWU/mzazi/mwanajamii kuunga mkono SIT na kushirikiana na SIT ili kukusaidia skuli kuwa jumuishi zaidi.
- Pia wakumbushe JWWU kwamba wamepokea mafunzo zaidi na kujengewa uwezo zaid kuliko wengi miongoni mwa wanachama mmoja mmoja wa SIT kwa hivyo wako katika nafasi nzuri ya kutoa maarifa na ujuzi wao kuhusu maana ya elimu mjumuisho.
- Watake washiriki kukaa kwa jozi (wawili wawili) kujadili swali lifuatalo: **"Jumuiya yako inawezaje kuongeza thamani/mchango kwa kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ?"**

Wakati wa kujibu swali hili wahimize washiriki kurejea vikwazo vilivyobainishwa siku iliyotangulia wakati wa kujadili 'jinsi gani kamati ya elimu mjumuisho ya skuli inaweza kukusaidia kutatua vikwazo vya ujumuishi'. Wahimize kufikiria juu ya faida ambayo jumuiya yao inayo kuhusiana na uhusiano wake na jamii na wazazi/walezi.

- Baada ya muda mfupi wakaribishe washiriki wote kutoa maoni yao na uyaandike katika flipuchati.

## PawaPointi Kushirikiana na SIT

- Onesha slaidi ya 4 ya PawaPointi. Waambie washiriki wajigawe katika vikundi vidogo vidogo (katika ngazi ya kitaifa waingie katika vikundi vya **wilaya/mkoa**). Katika vikundi vyao waambie washiriki waongezee juu ya mjadala uliopita na kufikiria kuhusu hali katika wilaya zao, na wajadili maswali yafuatayo na waandike majibu yao kwenye flipuchati:
  - Je, kuna fursa gani za wewe kujihusisha na kusaidia SIT katika wilaya yako?
  - **Je, ni vikwazo gani mahususi vya elimu mjumuisho unavyofikiri taasisi/jamii yako inaweza kusaidia kushughulikia?**
  - **Je, shirika/jumuiya yako linawezaje kusaidia SIT ili kudumishwa zaidi ya muda uliopangwa wa mradi?**
- Waambie vikundi vidogo sasa vijiunge na kikundi kingine kidogo ili kuunda kikundi kikubwa zaidi, (washiriki katika mafunzo ya ngazi ya kitaifa wanapaswa kuingia katika ‘timu zao za uwezeshaji’, k.m. Gardo au Kismayo n.k.)
- Waambie washiriki katika vikundi vipya walinganishe mawazo yao.
- Simamia mjadala wa pamoja kwa dakika chache kwa kuchukua mrejesho kutoka baadhi ya vikundi/ timu za uwezeshaji.

# Somo la 5: Jukumu la Mratibu wa elimu mjumuisho ya skuli

## Ujumbe muhimu

Sehemu kuu ya jukumu la mratibu wa elimu mjumuisho ni kuanzishana kushajiisha mashirikiano ya kujenga ujumuishi. Mratibu hutekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mikutano ya elimu mjumuisho ndani ya skuli na kufanya ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ili kuhakikisha kwamba inatekelezwa katika skuli hiyo. Hatafanya kazi zote peke yake. Kwa mfano, hahusiki na kuwabaini na kuwatathmini wanafunzi au hatakuwa na jukumu la utoaji wa vifaa na vitu vyengine kama vile vifaa saidizi.

## Maelezo ya usuli kwa mwezeshaji:

Somo hili linakusudiwa kutoa uelewa wa wazi wa jukumu muhimu la Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli katika skuli jumuishi na jamii. Washiriki wataelewa kuwa Mratibu huyu hawajibikii kufanya kazi zote za ujumuishi peke yake. Ana jukumu la **kuratibu;** hii ina maana, kufanya kazi na kamati za elimu mjumuisho za skuli, kuandaa na kusimamia, badala ya kuwa na wajibu kamili wa, kubaini, kutathmini na kufanya mengine yote mazuri yanayohusiana na ujumuishi.

Kwa vile nafasi hii ya Mratibu ni muhimu katika elimu, ni vyema kutambua aina ya mtu ambaye angefaa zaidi katika jukumu hili; si lazima mtu aliye katika nafasi kubwa zaidi au mwenye sifa nyingi zaidi za kitaaluma. Mratibu huyu ni lazima awe na nia ya kutoa fursa kamili kwa wanafunzi wote. Anapaswa kuwa mfano mzuri wa kuigwa na anayeweza kuwahamasisha wengine, huku akielewa mahitaji ya wenzake pamoja na wanafunzi.

Washiriki wanaweza kutaka kujua wakati wa somo hili, ikiwa kamati ambazo tayari zimeanzishwa katika skuli za majaribio zinao Waratibu wa elimu mjumuisho. Inafaa kujua ni skuli zipi zinao Waratibu na taarifa hii iwasilishwe kwa washiriki wakati wa somo hili.

### Katika kipindi hiki washiriki:

- Watajifunza jukumu la mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli

ü Watajadili jinsi Mratibu anavyotakiwa kuunda mtandao wa usaidizi katika skuli jumuishi na jamii kwa kuunganisha wadau katika ngazi za jamii, skuli na sera.

## Shughuli 5.1: Jukumu la mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli

1 dakika 45

Shughuli hii inampa kila mshiriki fursa ya kutafakari na kujadili anachofanya na asichofanya mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli.

### Maelekezo

- Wakumbushe washiriki kwamba kuna haja ya jukumu la kuratibu katika kamati ya elimu mjumuisho ya skuli (hili lilitajwa katika somo lilichopita).

PawaPointi **Somo la 5: Jukumu la mratibu wa elimu mjumuisho**

- Onesha slaidi ya 1PawaPointi ya Somo la 5. Waombe washiriki kufanya kazi wawili wawili na kujadili uelewa wao wa maana ya Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli. Kila jozi waandike sentensi moja kueleza wanachoelewa kuhusu Mratibu huyo.
- Baadae washiriki waoneshane na kuzijadili sentensi hizo katika vikundi vidogo vidogo.
- Mwishowe, watake vikundi vitoe mrejesho kwa washiriki wote kwa pamoja.
- Baada ya kila mtu kupata fursa ya kutoa maoni, waoneshe yafuatayo kwenye flipuchati (au kwenye slaidi ya 2 katika Somo la 5,) ambayo yanaelezea kile ambacho Mratibu huwa anafanya.

PawaPointi **Somo la 5: Jukumu la mratibu wa elimu mjumuisho**

- **Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli ni jukumu la kujitolea.**
- **Mratibu anapaswa kufanya kazi katika jukumu la kuratibu; hii ina maana ya kuandaa na kusimamia, badala ya kuwa na wajibu kamili, wa utambuzi, tathmini na utoaji wa elimu mjumuisho.**

- **Anapaswa kuwa mwanachama wa kamati ya elimu mjumuisho ya skuli na atasaidia kufanya kazi kuelekea sera na matendo jumuishi katika skuli.**

- Kauli hizi hizi pia zioneshwe ukutani ziwezekurejelewa wakati wote wa mafunzo. Waulize washiriki kama wangependa kuongeza chochote kwenye kauli hizi.
- Mpe kila mshiriki kadi nyekundu moja na ya kijani moja kama zile zinazotumiwa na waamuzi wa mpira wa miguu.
- Kisha soma sentensi moja kutoka katika **kauli zilizopo hapa chini** na mwombe kila mshiriki aoneshe kadi moja kutegemea kama anakubaliana au hakubaliani na kauli hiyo.

Kadi ya kijani inaonesha '**Kukubali'**

Kadi nyekundu inaonesha **'Kukataa'**

[**Tafadhali kumbuka**: shughuli hii pia inaweza kufanywa kwa kusogea kwenye mstari 'usioonekana' kwenye chumba cha mafunzo. Katika upande mmoja wa chumba kuna bango linaloonesha alama ya 'nakubaliana' na upande wa pili wa chumba kuna alama inayoonesha alama ya 'sikubaliani' na washiriki wasonge mbele kwenye mstari usioonekana kuelekea mwisho wa chumba kwa upande ambao wanakubaliana nao kulingana na majibu yao ya kauli hizo].

**Kauli za majadiliano**

- **Mratibu wa skuli lazima awe na ujuzi maalum kama vile Braille na Lugha ya Alama**

*(**Sikbaliani:** Mratibu SILAZIMA kuwa na ujuzi wa kitaalamu. Anafanya kazi kama mratibu kwa kuwaleta watu pamoja ili kujadili masuluhisho. Hii inaweza kuhusisha kuunganishwa na walimu waliobobea katika ujuzi fulani ikiwa wanapatikana lakini Mratibu haihitaji stadi hizi mwenyewe).*

- **Mratibu wa skuli ataweza kufanyakazi za kitaalamu za kupima uoni na usikivu**

*(**Sikubaliani**: kama ilivyo hapo juu)*

- **Mratibu wa skuli anapaswa kuwa katika kitengo au ofisi ya elimu kwa saa 8 kila siku ili kuhakikisha kwamba wazazi, walimu, n.k., wanajua mahali pa kumpata ikiwa wanahitaji ushauri wake.**

*(**Sikubaliani**: Jukumu la Mratibu ni jukumu la kujitolea na kwa hivyo ana uwezekano wa kuwa na kazi nyengine katika skuli au jumuiya. Anaweza*

*kupanga nyakati mahususi za mikutano anapopatikana kukutana na wazazi, walimu n.k.)*

- **Mwalimu ambaye ana uzowefu wa angalau miaka 20 ya kufundisha na aliye na sifa za juu kabisa za kitaaluma ndiye anayefaa kuchukuwa jukumu la Mratibu wa skuli.**

***(Sikubaliani** sifa muhimu zaidi ni kwamba Mratibu awe na shauku na aamini katika elimu mjumuisho. Jukumu hili pia linaweza kuchukuliwa na mwalimu au mfanyakazi wa utawala aliyehitimu hivi karibuni.)*

- **Mratibu wa skuli anapaswa kuhusisha wanafunzi na wazazi/walezi katika masuala mahususi kila inapowezekana.**

***(Kubali:** wanafunzi na wazazi/walezi ni baadhi ya wadau muhimu na walengwa wa kimsingi wa elimu mjumuisho. Kwa hiyo, wanapaswa kushirikishwa na kushauriana kila inapowezekana na inapofaa)*

- **Inawezekana kwa Mratibu wa skuli kuhusika katika kupanga shughuli za ziada kama vile michezo na maigizo.**

*(**Sikubaliani:** hili silo jukumu kuu la mratibu wa elimu mjumuisho, ikiwa shughuli za ziada zitakuwa na uzingatiaji maalum wa ujumuishaji basi mratibu atakuwa na jukumu la kupanga shughuli hizo)*

- **Mratibu wa skuli ni lazima ahudhurie mikutano ya SIT kila inapowezekana**

*(**Kubali:** kama mtaalamu wa elimu mjumuisho ni muhimu kwamba Mratibu ahudhurie mkutano wa SIT wakati wowote inapowezekana. Mratibu pia mara nyingi ataongoza katika kuhakikisha mikutano ya SIT inafanyika na hatua zinachukuliwa na zinafuatiliwa)*

- Baada ya kila kauli kusomwa na maamuzi kufanywa, wape muda washiriki kujadili kama kuna kutokukubalina kwa majibu yao. Wahimize washiriki kujaribu kubadilisha maoni ya kila mmoja na kusikilizana.
- Shughuli hii imeundwa ili kuwatia moyo washiriki kufikiria juu ya jukumu la Mratibu wa elimum mjumuisho wa skuli katika skuli zao na jamii. Pia ni nzuri sana kwa kukupa ufahamu kuhusu maoni ya washiriki kuhusu elimu mjumuisho.

## Shughuli 5.2: Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli kutoka Zambia akielezea uzowefu wake

1 dakika 30

### Maelekezo

- Waulize washiriki iwapo wanakumbuka jina la Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli kutoka Zambaia walipoangalia video hapo kabla.
- Jina lake lilikuwa **Bibi Marvellous Mubi.** Waambie washiriki kwamba watatazama sehemu nyengine ya video ya mahojiano na Bibi Mubi ili kujua zaidi kuhusu jukumu lake na wanapotazama wanapaswa kufikiria kuhusu maswali yafuatayo (pia kwenye Pawaointi slaidi ya 4)

PawaPointi

**Somo la 5: Jukumu la mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli**

- **Ni shughuli gani anazofanya Bibi Mubi akiwa ni Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli?**
- **Anashrikiana na nani?**
- **Nini maana ya 'Chumba cha Usaidizi wa Kijifunza' na Mpango Binafsi wa Kielimu (IEP)?**

- Onesha video. Urefu wake ni zaidi kidogo ya dakika 4. Baada ya washiriki kutazama wape dakika chache kujadili maswali wakiwa wawili wawili.
- Katika mjadala wa pamoa waombe baadhi ya washiriki kuwasilisha majibu yao. Rejelea vidokezo hapa chini inapohitajika.

## Maelezo ya Mwezeshaji: majibu ya maswali kutoka katika mahojiano ya Bi Mubi

**Ni shughuli gani anazofanya Bibi Mubi akiwa ni Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli**

- Kuratibu mipango ya elimu mjumuisho
- Kupanga shughuli za SIT
- Kuanzisha msingi wa usaidizi wa kujifunza
- Kutengeneza na kurekebisha nyenzo za kufundishia na kujifunzia
- Kusaidia katika mahitaji ya mtu binafsi ya watoto kujifunza
- Kukutana na wazazi/walezi ili kujadili tatizo la mtoto au kutoa ushauri/ kushajiisha wazazi/ walezi
- Kuratibu mikutano ya walimu
- Kuandaa Mipango Binafsi ya Kielimu

**Anashirikiana na nani ?**

- Wanafunzi
- Walimu
- Wazazi/walezi
- Wanajamii- Wajumbe wa SIT

**Ni nini Chumba cha Usaidizi wa mwanafunzi?**

Chumba kilichoo skuli ambapo shughuli mbalimbali za elimu mjumuisho zinaweza kufanyika - k.m. kutoa msaada wa ziada kwa mwanafunzi ikihitajika au walimu kuzalisha nyenzo za kufundishia na kujifunzia pamoja

**Je, 'Mpango wa Binafs wa Kielimu (IEP) ni nini?**

Mpango binafsi wa kielimu kwa mwanafunzi anayehitaji msaada wa ziada kuhusu jinsi skuli inavyoweza kumsaidia mwanafunzi huyo kuendelea katika kazi yake ya kitaaluma.

KUMBUKA: Chumba cha Usaidizi wa Mwanafunzi na Mpango Binafsi wa Kielimu unaangaliwa kwa undani zaidi kama sehemu ya kipengele cha Mafunzo ya Ualimu ya Elimu Mjumuisho (IETT) - hivyo mwalimu katika skuli za majaribio atafunzwa na kufahamu dhana hizi.

## Shughuli ya 5.3: Kazi za Mratibu wa Elimu Mjumuisho katika jamii, skuli, na wizara ya elimu/ ngazi ya sera

1 dakika 45

Mratibu wa skuli ndiye kiunganishi kikuu kati ya wanafunzi, familia, jamii, skuli na wataalamu wengine ambao wataunda mtandao wa usaidizi kwa skuli na jumuiya. Shughuli hii inawahimiza washiriki kufikiria kuhusu njia ambazo Mratibu wa skuli anaweza kuwa na ufanisi na ushawishi katika ngazi zote.

Washiriki wanaweza kuhitaji usaidizi/'vidokezo' kuhusu shughuli hii hasa ikiwa wana uzoefu mdogo wa skuli/sera. Jaribu kuhakikisha mchanganyiko wa washiriki katika kila kikundi unaojumuisha maarifa/uzowefu mbalimbali.

### Maelekezo

- Wagawe washiriki katika vikundi vitatu.
- Andika vichwa vya maneno vitatu katika ubao/flipuchati:
    - ü skuli, pamoja na SIT
    - ü jamii
    - ü Wizara ya Elimu na Michezo/ katika ngazi ya kisera.
- Kipe kila kikundi kimojawapo cha vichwa vya maneno vitatu na uwaambie **watatayarishe 'bango'** kuonesha jinsi Mratibu wa skuli anavyoweza kufanya kazi katika ngazi hii. Wanapaswa kuchora na kuandika mawazo yao kwenye flipuchati. Mawazo yanapaswa kuwasilishwa kwa uwazi ili wengine waweze kuyasoma / kuyaona.
- Kwa mfano: kikundi cha 2 ni jamii. Kikundi hiki kinapaswa kujadili hatua mahususi za jinsi Mratibu wa skuli anavyweza kufanya kazi na jamii na manufaa ya ushirikiano wa skuli na jamii.
- Wajulishe washiriki kwamba hakuna majibu sahihi au yasiyo sahihi kwa shughuli hii. Kile ambacho mara nyingi kitafanya kazi vizuri katika skuli moja au jumuiya moja huenda kisifanye kazi kwa skuli au jumuiya nyengine. Pia wanapaswa kufikiria kuhusu **mkabala wa mbinu pacha** ya kujifunza wakati wa kujibu swali - waoneshe mchoro wa mkabala wa mbinu pacha unaooneshwa kwenye chumba cha mafunzo (yaani wanapaswa kuzingatia shughuli za kumsaidia mwanafunzi mmoja mmoja na pia shughuli zinazoangalia kubadilisha 'mfumo').

- Baada ya dakika 20 au baada ya vikundi kumaliza kuandaa mabango yao, waambie kila kikundi kiwasilishe mawazo yao moja baada ya moja.
- Ruhusu muda wa majadiliano ya jumla baada ya kila mojawapo ya mawasilisho matatu. Tumia **Kielelezo 5.3** kuangalia mapendekezo yote na kuongeza chochote ambacho kinakosekana, pamoja na mawazo yako mwenyewe. Andika kila nyongeza kwa uwazi ubaoni/flipuchati.

**Kielelezo** **Shughuli ambazo Mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli anaweza kushiriki**

Hatimaye toa **Kielelezo 5.3** kwa washiriki ili wakisome.

# Somo la 6: Fursa za ushirikiano katika jamii zetu

## Ujumbe muhimu

Kutengeneza mtandao imara wa usaidizi wa elimu mjumuisho ni muhimu sana kwa skuli na kamati zao za elimu mjumuisho. Jumuiya za Watu wenye Ulemavu zina jukumu muhimu katika kujenga na kudumisha mitandao hii. Ili kujenga mitandao imara katika jamii zetu kwanza tunatakiwa KUANGALIA ni aina gani ya mali zilizopo katika jamii na KUFIKIRI ni jinsi gani tunaweza kuzitumia ili kusaidia kujenga uhusiano ulio imara kwa ajili ya elimu mjumuisho katika jamii.

## Maelezo ya usuli kwa mwezeshaji

- Ingawa ni muhimu sana kwa washiriki kuelewa vikwazo vya elimu mjumuisho vilivyopo katika jamii zao, ni muhimu pia kwao kutambua kwamba kuna mambo mengi mazuri yaliyopo katika jamii zetu ambayo tunaweza kuyatumia kusaidia elimu mjumuisho.
- Tunaweza kuona mambo haya chanya kama nguvu ambazo zitasaidia kuvunja vikwazo hivi na kuimarisha uwezo wa skuli katika elimu mjumuisho. Nguvu hizi zinaweza kuzingatiwa kama mali au kitu cha thamani katika jamii.
- Somo hili litawasaidia washiriki kuelewa jinsi mali hizi zinavyoweza kuwa watu mahususi na maarifa na uzoefu walio nao; zinaweza kuwa rasilimali halisi kama vile majengo au huduma zinazoweza kutumika kwa njia tofauti; au zinaweza kuwa mashirika ambayo yanaweza kuwa washirika katika kusaidia kuongeza ufahamu na kujenga uwezo wa kamati za elimu mjumuisho za skuli
- Somo hili litaTAZAMA na KUFIKIRIA kuhusu mali zilizopo katika jamii ambapo skuli za majaribio ziko kwa kuwatambulisha washiriki kwenye ramani ya mali ya jamii. Wanaweza kutumia ramani hii kubaini mali za elimu mjumuisho katika jamii yao.
- Somo hili pia litazingatia umuhimu wa ushirikiano mzuri ili kupata na kuimarisha mali hizi na kutafakari jinsi tunavyoweza kufanya kazi ili kudumisha madaraka hizi ndani ya jamii.

**Katika somo hili washiriki:**

- ü Watachunguza mali ya jumuiya ni nini na kwa nini ni muhimu kwa elimu mjumuisho
- ü Jifunze kuhusu uchoraji wa ramani ya mali za jamii kama njia ya kubaini ni mali gani iliyopo katika jamii zetu na kufikiria jinsi zinavyoweza kusaidia elimu mjumuisho.
- ü Tafakari juu ya matendo ya ushirikiano mzuri katika kuzifikia na kuimarisha mali hizi

## Shughuli 6.1: Tunaona nini tunaopoitazama jamii yetu?

1 dakika 60

### Maelekezo

- Hakikisha kwamba kila mtu ana angalau vipande vitatu vya karatasi (A4 iliyokatwa vipande viwili)
- Hakikisha kuwa kila mtu ana vikaratasi/kadi 10 hivi za manjano na 10 za bluu (au rangi zozote mbili tofauti)
- Hakikisha kuwa kuna gundi au kitu wanachoweza kutumia kubandikia karatasi ukutani
- Onesha kila mmoja picha tatu kwenye PawaPointi (slaidi ya 1) au toa nakala za picha tatu kutoka **Kielelezo 6.1** - picha moja kwa kila karatasi ya A4 kwa vikundi vya washiriki.

**PawaPointi** **Somo la 6: Picha za jamii**

au

**Kielelezo** **Somo la 6: Picha za jamii**

- Onesha slaidi ya 2 pamoja na swali hili au andika katika flipuchati

**Unapotazama hizo picha tatu unaona nini?**

- Mwambie kila mtu aandike neno moja ambalo anafikiria kwanza anapotazama kila moja ya picha hizo. Washiriki waandike kila neno kwenye kipande tofauti cha karatasi (maneno 3 - moja kwa kila Waeleze washiriki kwamba linaweza kuwa neno lolote wanalofikiria wanapotazama picha (hakuna maneno sahihi au yasiyo sahihi)
- Wanapomaliza kutazama picha na kuandika maneno yao, waambie washiriki wakabandike maneno yao ukutani. Wanaweza kuzibandika mahali popote wanapopenda kwenye ukuta wa chumba cha mafunzo.
- Waombe washiriki kuzunguka chumba na kuangalia maneno yote tofauti ambayo kila mtu ameandika.
- Waambie wafikirie kwa makini ikiwa wanafikiri kwamba neno hilo linaelezea tatizo au kitu ambacho si sahihi (hasi) au kama linaelezea jambo ambalo ni zuri (chanya)
- Eleza kwamba kama wanadhani neno ni hasi basi waweke bango la njano kwenye karatasi na kama wanadhani neno hilo ni chanya weka bango la bluu juu yake.
- Mara baada ya kila mtu kuweka karatasi/kadi yake kwenye maneno waambie wakae chini
- Sasa mwambie mmoja wa wawezeshaji wengine kupanga upya maneno ukutani ili maneno yote hasi yawe pamoja na maneno chanya yote yawe pamoja.
- Ukishafanya hivi waulize kama kuna jambo lolote wanaloliona kuhusu maneno hayo
  - Je, mara nyingi kuna maneno chanya au hasi?
  - Ni nini kinachodhihirika kutoka katika maneno hasi?
  - Ni nini kinachodhihirika kutoka katika maneno hasi?
- Tu unapokuwa na majadiliano weka Slaidi ya 3 na upitie hoja zifuatazo kuhusu kuhama kutoka kwa matatizo hadi mali

**PawaPointi** **Somo la 6: Kutoka matatizo hadi mali**

- Ijapokuwa ni muhimu kila mara kuangalia matatizo au makosa katika jamii na kuelewa ni kwa jinsi gani haya yanaweza kuwa vikwazo vya elimu mjumuisho, kwa mfano, umaskini, ni muhimu pia kufikiria mambo katika jamii yanayoweza kusaidia kuondoa vikwazo hivi na kuimarisha uwezo wa skuli kwa ajili ya elimu mjumuisho

- Tunaweza kuona mambo haya chanya kama nguvu au kitu cha thamani ndani ya jamii - tunaweza kuyaita **MALI**
- Raslimali katika jamii zinaweza kusaidia kuondoa vikwazo vya elimu mjumuisho au zinaweza kusaidia kuleta mabadiliko.
- Tunaweza kutumia mali katika jamii kusaidia SITs na kusaidia kuongeza uelewa kuhusu elimu mjumuisho.

- Sema kwa washiriki kwamba sasa tutaangalia na kufikiria zaidi kuhusu mali

## Shughuli 6.2: Kuna aina gani za mali?

1 dakika 45

### Maelekezo

- Waeleze washiriki kwamba sasa tutafikiria jinsi tunavyoweza kubaini mali katika jumuiya yetu ambazo zinaweza kuwa vyanzo muhimu vya usaidizi wa elimu mjumuisho.
- Waulize washiriki kama kuna mtu yeyote anaweza kutoa mfano wa 'rasilimali ya jamii' na kueleza kwa nini wanafikiri ni rasilimali - chukua mfano mmoja au miwili.
- Mkumbushe kila mtu kwamba rasilimali ni nguvu au kitu cha thamani ndani ya jamii, ambacho kinaweza kuwa na manufaa kwa jamii - sema kwamba rasilimali inaweza kuwa mtu au watu, inaweza kuwa rasilimali ya kama ukumbi wa jumuiya au msikiti , au inaweza kuwa shirika - weka maelezo ya jumla katika hatua hii.
- Waombe washiriki sasa wajipange katika vikundi. Kuwe na watu 4 katika kila kikundi
- Toa kwa kila kikundi nakala ya mchoro wa kina wa jamii (**Kielelezo 6.2**)
- Waambie waangalie kwa makini picha na wajadili maswali yafuatayo (kwenye Slaidi ya 4).
    - Je, ni mali gani unaweza kuona kwenye picha ambayo inaweza kuwa muhimu kama msaada au nyenzo kwa kamati za elimu mjumuisho za skuli?
    - Rasilimali hizi zingewezaje kusaidia kukabiliana na vikwazo vya elimu mjumuisho ambavyo walivitambua na kujadiliwa siku moja kabla (onesha ukuta ambao walitengeneza)

- Je, mali hizi zinaweza kuwa msaada au rasilimali kwa SITs?

- Wape vikundi dakika 25 kujadili maswali hayo
- Kiambie kila kikundi kielezee kwa ufupi mali walizoweza kuona kwenye picha na jinsi mali hizo zinavyoweza kusaidia SIT na kusaidia kujenga elimu Mjumuisho.
- Andika mali watakazozitaja katika flipuchati.
- Sasa rudi kwenye Slaidi ya 1 (picha tatu) au waambie watazame tena picha tatu walizozitazama kwanza na kuona kama wanaweza kuona "mali" yoyote katika picha hizi - ongeza chochote kinachokuja kwenye flipuchati.
- Sasa onesha Slaidi ya 6 ya PawaPointi na pitia nukta zifuatazo kuhusu aina za mali zinazopatikana katika jamii.

**PawaPointi** **Somo la 6: Mali ni nini?**

- Mali inaweza kuwa ujuzi wa vitendo (kwa mfano, useremala)
- Rasilimali inaweza kuwa maarifa ya kitaalamu ambayo mtu anayo (kwa mfano, maarifa ya mhadhiri wa chuo kikuu)
- Raslimali inaweza kuwa nia au shauku ambayo mwanajamii anayo, kwa mfano, timu ya soka ya mtaani.
- Raslimali inaweza kuwa nyenzo katika jamii (kwa mfano, msikiti au sehemu ya kulia ambapo watu wanaweza kukutana)
- Raslimali inaweza kuwa shirika/jumuiya iinalofanya kazi katika jamii (kwa mfano, shirika ya wanawake)
- Mali inaweza kuwa mtu mwenye ushawishi katika jamii, kama vile Imamu.
- Ingawa mali nyingi ziko wazi kwetu, wakati mwengine haziko wazi, na tunahitaji kufikiria kwa ubunifu kuhusu jinsi mtu au kitu kinavyoweza kuwa rasilimali inayowezekana.


- Uliza kama kuna maswali yoyote kutoka kwa yale uliyowasilisha kwenye slaidi.
- Waambie washiriki kwamba sasa tutafikiria juu ya kile tumejifunza ili kutengeneza ramani ya rasilimali zote zinazowezekana za elimu mjumuisho zilizopo katika jamii zetu.

## Shughuli 6.3: Kuandaa ramani ya mali za jamii

1 dakika 120

Dakika 5 za utangulizi na maelekezo.
Dakika 45 za kuunda ramani.
Dakika 40 kwa kutoa mrejesho na majadiliano.
Dakika 30 kwa majadiliano ya jumla

- Waambie washiriki wajipange katika vikundi vyao vya wilaya/mkoa (ili watu wote kutoka wilaya/mkoa mmoja wakae pamoja)
- Hakikisha kwamba kila kikundi kina karatasi kubwa ya flipuchati ya A3 na kalamu za rangi tofauti za kuchora na kuandika.
- Waambie washiriki kwamba sasa tutaunda ‘ramani ya rasilimali’ za jamii yetu
- Waoneshe Slaidi ya 7 inayoelezea jinsi ya kutengeneza ramani ya mali ya jamii
- Kisha waoneshe Slaidi ya 8 inayoonesha baadhi ya mawazo ya kuwasaidia kufikiria kuhusu mali katika jamii zao
- Kisha waoeshe Slaidi ya 9 inayoonesha mfano wa ramani ya mali za jamii




Mfano wa ramani ya mali za jamii

[Ufafanuzi wa picha: Katikati ya kipande cha karatasi kuna maduara matatu yaliochorwa kwa mkono yaliyopangwa katika umbo la pembe tatu. Katika duara la kwanza upande wa kushoto pameandikwa neno "watu". Duara jengine limeandikwa "jumuiya" na la tatu lina maneno "rasilimali zinazoonekana". Maduara matatu yameunganishwa pamoja kwa mistari myeusi].

Katika mzunguko wa duara la "watu" kuna maduara madogo madogo manne yote yameunganishwa na duara hilo kwa mstari mweusi. Katika moja kati ya maduara haya madogo kuna kikongwe aliyeshika fimbo na chini yake pameandikwa ndani ya duara "Bw. P. mwalimu mstaafu" na chini ya maneno haya katika mabano pameandikwa "husaidia kuzungumza na wazazi". Duara jengine katika maduara madogo kuna picha ya kijana wa kike akiwa amekaa anashona kwa kutumia cherehani na chini yake pameandikwa "Mama K. mshoni". Duara jengine dogo lina maneno "Imam msikitini". Katika duara jengine dogo kuzunguka duara la watu kuna picha ndogo ya kibanda kilichoezekwa bati. Nje ya kibanda kuna watu waliokaa kwenye meza. Wawili wanazungumza na mwengine amekaa anakula. Kuna birika nyuma yake inachemka jikoni.

Kuzunguka duara la “jumuiya” kuna maduara madogo matatu yaliounganishwa na duara hilo kwa mstari mweusi. Duara dogo la mwanzo lina picha ya dereva wa bodaboda na chini yake pameandikwa “Chama cha madereva wa Bajaj”. Duara jengine dogo lina picha ya kikundi cha watu waliokaa wanazungumza. Chini ya picha pameandikwa “Kikundi cha Vijana” na kwenye mabano pameandikwa “husaidia kusambaza machapisho”.

Kuzunguka duara la rasilimali kuna maduara sita madogo yaliouganishwa na mstari mweusi. Katika duara la kwanza kuna picha ya skuli. Duara jengine dogo lina picha ya mwanamke anayeuza matunda na mboga mboga chini yake pameandikwa “Soko la Mboga mboga” na “Miche kwa ajili ya Skuli” katika mabano. Duara jengine dogo lina picha ya kanisa. Duara jengine dogo lina picha ya dereva wa bodaboda aliyepakia abiria. Chini ya picha hii pameandikwa “madereva wa bodaboda” na neno “usafiri” katika mabano. Kuna maduara mengine madogo mawili yaliounganishwa na maliasili – moja lina neno “ziwa” na jengine lina neno “ardhi”.

PawaPointi

## Somo la 6: Ramani ya mali ni nini?

- Waulize kama kuna yeyote ana maswali kuhusu kazi hii au maoni yoyote
- Waambie kwamba watakuwa na dakika 45 za kufanyia kazi ramani zao
- Wakumbushe kwamba hawapaswi kunakili tu kile walichokiona kwenye picha - wanapaswa kujaribu na kufikiria watu mahususi, rasilimali au mashirika katika jamii yao wenyewe.
- Tembea chumbani huku kila mmoja akifanyia kazi ramani yake ili kujibu maswali yoyote watakayokuuliza
- Baada ya dakika 40 wakumbushe wote kuwa wamebakisha dakika 5 kumaliza ramani zao
- Baada ya dakika 5 kuisha, waambie waende kubandika ramani zao ukutani
- Sasa eleza kwamba wilaya mbili/mikoa miwili wakae pamoja na kuwasilisha ramani zao kwa kila mmoja, kuuliza maswali na kujadili mfanano au tofauti zozote.
- Vipe vikundi kama dakika 40 hivi kwa mawasilisho na majadiliano yao
- Sasa warejeshe wote pamoja na wezesha majadiliano juu ya maswali yafuatayo (dakika 30)

- Je, ilikuwa vigumu kiasi gani kufikiria ni mali gani iliyopo katika jamii yetu?
- Je, kulikuwa na vitu muhimu katika michoro ya vikundi vyengine ambavyo hukuvifikiria?
- Unafikiri ni kwa nini ni muhimu KUTAZAMA na KUFIKIRI kuhusu mali katika jamii zetu?

## Shughuli 6.4 Kuimarisha mali za jamii kupitia mashirikiano sahihi

1 dakika 60

### Maelekezo

- Wakumbushe washiriki kwamba kabla ya chakula cha mchana tulijifunza kuhusu mali/rasilimali za jamii na tukafikiria kuhusu mali zilizopo katika jamii zetu.
- Eleza kwamba kutambua na kuthamini mali za jamii zetu ni hatua ya kwanza, lakini pia tunahitaji kufikiria jinsi tunavyoweza kujenga mtandao thabiti wa mali za jamii ambayo unaweza kusaidia kamati za elimu mjumuisho za skuili na kusaidia kujenga elimu mjumuisho.
- Sema kwamba katika somo hili tutafikiria jinsi ya kufanya hivyo kwa ushirikiano wenye ufanisi
- Anzisha mjadala kwa kuwauliza watu kwa nini wanafikiri ushirikiano katika elimu mjumuisho ni muhimu
- Tumia kama dakika 10 kutafakari hili na kisha eleza kwamba ingawa ushirikiano ni muhimu, si rahisi kila wakati. Sema kwamba sasa tutaandaa maigizo kuhusu ushirikiano ili kufikiria kuhusu matendo mazuri na mabaya.
- Wagawe washiriki katika vikundi - idadi katika kila kikundi itategemea idadi ya washiriki, lakini kuwe na kiasi watu 4 au 5 katika kila kikundi.
- Kipe kila kikundi mojawapo ya matukio kutoka kwenye **Kielelezo 6.3.**

**Kielelezo** **Somo la 6: Matukio/visa vya maigizo-dhima**

- Weka Slaidi ya 10 yenye nyuso mbili (au zichore kwenye flipuchati) na mwambie kila mtu kunakili nyuso zote mbili kwenye karatasi mbili za A4 tofauti na uziweke kwa ajili ya baadaye.
- Eleza kwamba wana dakika 15 za kujadili na kufanya igizo dhima lao. Hakikisha kila kikundi kinaweka wazi jukumu la mwanachama wa JWWU wakati wanaigiza.
- Wakati washiriki wanapanga maigizo dhima yao, tayarisha chumba kwa ajili ya maigizo dhima, tafuta eneo la 'jukwaa' na wenyeviti wa vikundi katika eneo la 'hadhira'.
- Baada ya dakika 15, kila kikundi kiwasilishe igizo dhima lao, ambalo halipaswi kuwa zaidi ya dakika 5.
- Kabla ya maigizo dhima kuanza, waeleze washiriki (hadhira) kwamba wanapotazama wanapaswa kuinua uso mmoja kuonyesha kama wanahisi anachofanya mshiriki katika igizo dhima ni kitendo kizuri au kibaya.

  J Mwanachama wa JWWU anaonyesha kitendo kizuri (chanya)

  L Mwanachama wa JWWU anaonesha kitendo kibaya (hasi)

- Kabla ya igizo dhima kuanza, chora safu wima tatu kwenye flipuchati – juu ya safu wima moja andika 'chanya', inayofuata andika 'hasi' na kwenye safu ya mwisho andika 'sina na uhakika'.
- Wakati maigizo dhima yanafanyika, weka kwenye flipuchati tabia ambazo watu walisema ni hasi na zile ambazo zilikuwa chanya.
- Ikiwa kuna tabia yoyote ambapo hadhira inaonesha nyuso chanya na hasi, andika tabia hizi kwenye safu 'sina uhakika'.
- Baada ya maigizo dhima kukamilika waambie kuwa kila mtu atafakari juu ya tabia ulizoziweka kwenye bango. Ongoza mjadala kwa kuuliza:
  - Kwa nini watu walifikiri kwamba tabia katika safu hasi hazikuwa sahihi?
  - Kwa nini watu walifikiri kwamba tabia katika safu chanya zilikuwa sahihi?
  - Kuwa na majadiliano juu ya tabia hizo ambapo watu walihisi tofauti - jaribu kufikia makubaliano kuhusu tabia zilizo hasi au chanya.

## Shughuli 6.5: Kudumisha mtandao imara wa mali za jamii

1 dakika 45

- Anzisha mjadala wa kipindi hiki kwa kumshukuru kila mmoja kwa igizo dhima na wao kubaki katika vikundi walivyokuwa katika igizo dhima.
- Sasa uliza kama kuna mtu yeyote anaweza kutoa mfano wa watu katika jamii yao (au katika jamii nyengine wanayoijua) walioshirikiana vyema kuleta aina fulani ya mabadiliko. (Unaweza pia kutoa mfano wako mwenyewe ili kuendeleza mjadala)
- Tumia kama dakika 10 kuruhusu watu kutoa mifano yoyote na kufanya kila mtu afikirie kwa nini mifano hii ilifanikiwa
- Eleza kwamba sasa tutafikiria jinsi tunavyoweza kuendeleza ushirikiano tunaotaka kujenga kati ya mali za jamii na kamati za elimu mjumuisho za skuli.
- Mkumbushe kila mtu kuhusu video tulizoziona kutoka Zambia na changamoto ambazo watu walitaja kuhusu kudumisha kamati za elimu mjumuisho za skuli baada ya mradi kumalizika na mahusiano ambayo yalikuwa yamejengwa ili kusaidia elimu mjumuisho katika jamii zao.
- Onesha Slaidi ya 11 na uwaambie watu warudi kwenye vikundi vyao vya igizo dhima kujadili maswali haya (au andika maswali kwenye flipuchati)
    - Ni changamoto gani wewe (JWWU) unaweza kukabiliana nazo katika kudumisha uhusiano thabiti kati ya skuli na jamii?
    - JWWU inaweza kufanya nini katika kuzishughulikia changamoto hizi (kujaribu kuhakikisha kuwa chngamoto hizo hazitokei)?
- Acha vikundi vijadili maswali haya kwa takriban dakika 20 kisha waambie wajadiliane na washiriki wote kwa pamoja kile walichojadili katika vikundi vyao.
- Kwenye flipuchati andika changamoto ambazo watu walizifikiria na masuluhisho yoyote waliyoyajadili (dakika 15).
- Vikundi vinapomaliza kuwasilisha maoni yao, waulize kama kuna yeyote angependa kutoa maoni juu ya jambo lolote.
- Hitimisha somo hili kwa kuwakumbusha washiriki kuwa tunatakiwa daima kufikiria juu ya uendelevu katika upangaji wetu kwani elimu mjumuisho inahitaji muda na tunatakiwa kuhakikisha kwamba mradi ukishakamilika kile ambacho kimefanyika katika hakipotei na kinaendelezwa.

Moduli ya

# 2

# Vielelezo na vitini

# Kielelezo 1.2: Skuli ya msingi na sekondari ya Shungu, Zambia: Tafakuri kuhusu skuli jumuishi na jukumu la Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli

## Yafuatayo ni maelezo ya filamu

**Bw. Orgency Malumbe, Mwalimu Mkuu, Skuli ya Shungu Msingi na Sekondari**
**Nakusalimu**.
Naitwa Malumbe Orgency, mwalimu mkuu wa skuli ya Shungu, maandalizi, msingi na sekondari. Nimekua mwalimu mkuu wa skuli hii kwa miaka saba sasa. Nipo kwenye skuli hii tangu mwaka 2014, na kwa kushirikiana na jamii ya hapa, walimu, wazazi, makanisa, wafanyabiashara sokoni, tumeshirikiana pamoja kuhakikisha skuli yetu inafika hapa tulipo, kwa kuzingatia miongozo ya elimu mumuisho.

Kwa hivyo hii ni Shungu, ambayo ipo katikati ya kitongoji cha Maramba, ikizungukwa na Zeko, Malota, na sehemu ya kambi ya polisi. Ni sehemu ya kipekee kwa sababu skuli imezungukwa na moja kati ya jamii korofi sana. Jamii ambayo uhalifu ni wa kiwango cha juu kiasi, matumizi ya mihadarati na maovu mengine yanayotendeka katika jamii. Licha ya hayo kuna mengi yamefanyika katika programu ya elimu mjumuisho, tumeweza kuisaidia jamii na tumefanikiwa kama unavyoweza kuona pale, mita chache kutoka hapa skuli kuna kanisa. Tuna kanisa jengine pale na tunawatumia viongozi wa makanisa kutusaidia kuwarekebisha aina ya watoto tulionao.

Kwa hivyo elimu mjumuisho, tutakapoitekeleza kwenye skuli, inatekelezwa pia kanisani. Upande mwengine kule, kuna zahanati. Tuna zahanati, Zahanati ya Maramba, ikimaanisha kwamba kuna ufikiwaji rahisi wa huduma za afya kama skuli ambayo ni sehemu ya jambo hili, la ujumuishi. Nyuma yake, kuna soko ambalo ni mfano mzuri wa sehemu ya ujumuishi. Tuna uhusiano na ushirikiano mzuri na soko kuhusu jinsi ya kuwasimamia watoto wetu. Watoto wetu watakua skuli, mara wanakwenda kule, lakini mara hurejeshwa hapa skuli na baadhi ya viongozi wa lile soko.

**Bi Marvelous Mubi, Mratibu wa Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli, Skuli ya Shungu**

Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ni kamati ambayo tuliianzisha mnamo mwaka 2016 au 2017 na hii ni kamati ambayo imeshirikiana na skuli bila ya kuchoka mpaka hivi sasa. Kamati hii inajumuisha mwalimu mkuu mwenyewe, mwalimu mkuu msaidizi, tuna uwakilishi wa walimu wengine katika kamati, lakini pia tuna wawakilishi wa wanafunzi katika kamati. Na wajumbe wengine kutoka nje ya sekta ya elimu, au nje ya skuli tuna wawakilishi kutoka sekta ya afya, viongozi wa kanisa, wafanyakazi wa jamii, tuna wazazi wa watoto wenye ulemavu, wabunge, na pia jamii – hao ni baadhi ya watu wanaopatikana katika kamati hii.

Jukumu la kamati hii, ni kushirikiana na skuli ili programu ya elimu mjumuisho, au hii elimu mjumuisho iweze kuwa ya mafanikio kwa wanafunzi, walimu na wazazi. Kwa hivyo jukumu la kwanza la kamati hii lilikua ni uhamasishaji pale tulipoanza programu hii, walikua na itikadi zao, taratibu zao za maisha, kwa hivyo kulikua na kazi ya kuiendea jamii, kuwaelimisha watu kuhusu elimu mjumuisho ni nini. Walifundishwa kusema kwamba watoto wenye ulemavu hawapaswi kufungiwa majumbani, kuachwa nyumbani badala ya kuandikishwa skuli, au kwamba hawastahiki kupelekwa katika hizi zinazoitwa skuli za kawaida. Kwa hivyo walielimishwa kuhusu mambo hayo. Matokeo yake muitikio ulikua ni mkubwa mno, walijumuika nasi, wazazi kupitia uhamasishaji uliofanywa na kamati hii, wajumbe wa kamati hii. Na jambo jengine pia, jukumu lao ama walichokifanya ni kuandaa mradi, tulipokua tunaanza kuingia katika elimu mjumuisho, kwa kuwa miundombinu iliyokuwepo ilikua haikidhi mahitaji ya elimu mjumuisho. Kwa sababu hiyo tukalazimika kuja na miradi kama vile ujenzi wa njia rafiki na ngazi mtelezo (rampu) kuzunguka skuli, lakini pia kupaka rangi skuli, kuimarisha mwangaza madarasani, kuimarisha mwangaza katika vyoo, na hata eneo lote la skuli, kwa upande wa ngazi mtelezo, njia zenyewe, njia zilitakiwa ziwe rahisi kupitika.

Tunapokua katika kamati, tunashirikiana na wazazi kutoka kutoka nje, na tunapozungumzia wazazi kutoka nje, ni wale wazazi kutoka jamii inayotuzunguka. Kwa hivyo hata pale tunapoanza kwa kusema tunataka kushirikiana nao, tunataka watoto wenye ulemavu wahudhurie skuli, tunawataka wanafunzi waliotoroka skuli warudi, tunawataka watoto wote waliofikia umri wa kuandikishwa skuli waandikishwe. Ni kamati hii iliyotoka kuhamasisha watu, kuzungumza na wazazi, jirani zao, watu wanaoishi nao na ilikua rahisi kwao kufanya hivyo kwa sababu wanaishi nao na wanajuana. Kwa hivyo, waliwaleta baadhi ya vijana waliotoroka skuli, na waliwaleta watoto

wenye ulemavu skuli, hayo ni baadhi tu ya mambo waliyofanya. Lakini pia wamefanikiwa kutekeleza baadhi ya miradi kama kujenga ngazi mtelezo kuzunguka skuli, ni kazi ya Kamati kwa sababu tuna wazazi humu ambao ni mafundi, mafundi rangi, kwa hivyo hao ndio waliosaidia, ndio wanaokaa na kujadili mambo ya kufanya na hatimae wanachukua hatua …

**Mama Pauline Hatimbula, mama wa Daniel, mwanafunzi mwenye ulemavu anayesoma skuli ya sekondari Shungu**
Elimu mjumuisho imenisaidia. Watoto wangu walikua hawaendi skuli lakini elimu mjumuisho ilipoanza, mwanangu nilimuandikisha skuli. Leo hii mwanangu anafurahia elimu anayoipata hapa skuli ya sekondari Shungu.

… wamefanya mengi ambapo mwanangu, kama isingekua elimu mjumuisho asingeweza hata kusoma, sasa anaweza kusoma, hata kujumuika katika michezo. Anaweza kucheza mpira wa miguu na wenzake, hata kukimbia. Leo, kama isingekua skuli jumuishi, sidhani kama angeweza kufanya yote hayo. Anayafanya hayo kwa sababu ya elimu mjumuisho.

… kabla ya mwanangu hajajiunga na skuli hii jumuishi, mwanangu kwa kweli alikuwa anakabiliwa na changamoto kubwa, ambapo baadhi ya watu hawakuwa wakicheza nae, au kuzungumza nae. Alikuwa na wakati mgumu wa kunyanyapaliwa kwa sababu hakua huru hakua huru katika mambo yote aliyokuwa anatamani kufanya. Lakini hivi sasa yupo huru anaweza kufanya chochote anachojisikia.

… tulipoanzisha skuli jumuishi nakumbuka walitoa tangazo katika skuli ya sekondari Shungu, wakiwataarifu watu ambao wana watoto wenye ulemavu majumbani mwao, tukawaandikishe skuli kwa hivyo walituandikia tangazo wakitutaarifu kwamba skuli ipo kwa ajili yao kwa hivyo tusiwafiche watoto majumbani, kwa sababu baadhi ya watu wanawaficha watoto wao majumbani, wanawahudumia watoto wao majumbani na hawawaruhusu watoke lakini sasa tangu serikali ilipoanzisha …

**Bw. Orgency Malumbe, Mwalimu Mkuu, akizungumza na wanafunzi skuli**
“Sawa, kwa hivyo mnapoiangalia hii skuli, mnadhani ni rafiki kwa watu wenye ulemavu?”
“Ndio”
“Sawa, kwa hivyo ni vipi watu wanaotumia viti mwendo huweza kufika madarasani?”
“Kwa kusaidiwa na rafiki zao, ndio”

“Je! Madarasa yenu yamewekewa miundombinu kuwezesha kitimwendo kufika darasani?”
“Ndio”
“Wamewekewa kitu gani cha kuwawezesha kufika darasani?”
“Mtelezo”
“Mnaziita mtelezo?”
“Ndio, kitu cha kuteleza ambapo hata kitimwendo kinaweza kupita”
“Tunaziita rampu (ngazi mtelezo)”
“Ndio, ngazi mtelezo (rampu)”
“Nzuri sana. Mnawaonaje watu wanaotembea masafa marefu, masafa marefu kabisa. Kuna watoto ambao wanatoka Gebe, mnajua Gebe iko wapi?”
Hata Makuni
“Hata Makuni. Mnawaonaje? Hamuoni kwamba tumewatenga? Kwa sababu kila siku wanachelewa. Mmewahi kusikia kuwa kuna mtu yeyote hapa skuli ambae alipewa baskeli?”
“Hapana”
“Mwaka uliopita tuliwapatia, tuliwapatia kama vijana watatu hivi kutoka Gebe, inaitwaje ile sehemu nyengine inayofuata baada ya Linda, Maloni ndio, tuliwapa baskeli na bado wanaendelea kuzitunza. Wapo wanafunzi ambao wanakuja kwa baskeli”
“Ndio, nimewaona”
“Hizo ni baskeli za skuli. Ndio, lengo letu ni kwamba watakapomaliza skuli, kama walivyomaliza kundi la mwanzo. Walizirudisha baskeli skuli, baadae mwalimu mnasihi atawatambua wanafunzi wenye mahitaji kupitia wazazi, watawatambua wanafunzi wengine wanaohitaji baskeli ili waweze kuja skuli kwa wakati.”

“Lakini vipi kuhusu, nimekua nasikia taarifa kuhusu baadhi ya watoto ambao wanafanya kazi za bustani.”
Ndio.
Wanafanya kazi za bustani?
Ndio.
Kuna utaratibu gani sasa kuhusu hao watoto wanaofanya kazi hizo?
Utaratibu ni kwamba wanafanya kazi za bustani halafu hawalipi ada ya skuli. Pesa wanayoipata kutokana na kazi ya bustani ndio pesa wanayoitumia kulipa ada ya skuli.

**Bi Marvelous Mubi**
Kila mwanafunzi anahusika hapa, kwa maana ya kila mmoja, madarasa yote hata wale wanafunzi wanaoitwa ‘wa kawaida’, wenye ulemavu wote

wanahusika katika kumwagilia maji hizi, wakifanya hivyo kwa zamu wakimwagilia na kutunza bustani…

**Bi Marvelous Mubi**
Awali ya yote ni kwamba watu wanahitaji kufanya kazi pamoja kutoka katika maeneo tofauti. Kumbuka kwamba hapa tunafanya kazi na watu kutoka kwenye sekta ya afya, polisi, elimu, ustawi wa jamii, kwa hivyo huchangia mawazo tofauti, tukiangalia ujuzi tulionao. Tunajifunza mengi. Fundi seremala watakuwepo wakitoa mtazamo wao, kutoka sekta ya afya nao wataeleza mtazamo wao, kwa upande wetu sisi watu wa elimu tutaeleza mtazamo wetu, mwisho wa siku tutaweza kupata kile tunachokihitaji.

**Bi Marvelous Mubi**
Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ikiwa inaundwa na watu au wazazi ambao wanatoka katika jamii wanawajua watu waliopo katika hiyo jamii kwa sababu kama kuna jambo jipya na wewe unazungumza na watu unaowajua watakusikiliza na kutilia maanani unachokisema. Kwa hivyo wakiwatumia watu kutoka katika jamii yao watawasikiliza na kutekeleza kile unachokisema kama tulivyofanya katika skuli yetu tulipowapeleka wazazi katika jamii wanazotoka na kuwaelimisha wanajamii wenzao ambao walikuwa wanawajua huku wakijua ni mzazi yupi anahitaji kupata taarifa na watoto wepi wana ulemavu, ni mzazi yupi ana mwanafunzi au watoto mwenye ulemavu. Kwa hivyo walikua wanazungumza na watu ambao tayari walikua wanawajua kwa hivyo walipotuletea hapa kama walimu tuliongezea tu kile wazazi walichokianza.

**Mama Pauline Hatimbula**
… tafadhali tuwe wawazi kwa watoto wenye ulemavu, tukawaandikishe skuli, tuwape fursa ya kujifunza kwa sababu, wao ndio kesho yetu, hatujui nini mungu anaweza kukifanya katika maisha yao.

Tafadhali Shungu ni skuli nzuri, Shungu ni skuli nzuri kabisa ukitaka kumleta mwanao, mlete mwanao skuli ya sekondari ya Shungu na utafaidika!

# Kielelezo 1.3a Visa mafunzo – nini maana ya kamati za elimu mjumuisho za skuli?

**Soma visa mafunzo vifuatavyo. Unadhani kila kisa kinaelezea maana ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli? Kwa nini?**

**Kisa mafunzo A**
Kila baada ya miezi 3, walimu 3 wa madarasa katika skuli ndogo iliyopo kijijini hukutana kujadili changamoto zinazowakabili katika kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu walioandikishwa katika skuli hiyo. Walimu wengine wawili katika skuli hiyo hawapo tayari kujumuika na walimu hawa katika vikao, na hakuna mtu yeyote aliyewashawishi kushiriki katika vikao hivyo.

**Kisa mafunzo B**
Katika skuli kubwa, kuna timu iliyoundwa ili kuandaa mipango binafsi ya kielimu (IEP) kwa wanafunzi 30 ambao walibainika kuwa na mahitaji maalumu katika kujifunza. Timu hiyo inajumuisha mtaalamu wa mbinu za kufundishia, mwanasaikolojia, walimu wawili wa madarasa, na wataalamu 3 wa elimu mjumuishi kutoka nje ya skuli.

**Kisa mafunzo C**
Kila mwaka, Skuli C huitisha mkutano mmoja unaojumuisha wazazi wote/walezi. Katika mkutano huu, mwalimu mkuu huwaeleza wazazi/walezi kuhusu sera ya skuli ya elimu mjumuisho, akiwaomba kuhakikisha kwamba watoto wote wanahudhuria skuli, na kuwaambia kile ambacho walimu na wataalamu maalum wamekuwa wakikifanya ili kuwasaidia wanafunzi waliobainika kuwa na mahitaji maalum katika kujifunza.

**Kisa mafunzo D**
Skuli D ina wanafunzi tofauti, wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kujifunza/ulemavu na wanafunzi kutoka katika makabila matatu tofauti. Baadhi ya walimu, wazazi/walezi na wataalamu hukutana kila baada ya wiki mbili kujadili changamoto mpya zilizoibuka katika ujumuishaji, na kutathmini maendeleo na kutatua changamoto. Hivi sasa wapo katika mchakato wa kuwajumuisha wawakilishi wawili wa wanafunzi katika kikundi hicho, ili wapate mawazo kutoka kwa wanafunzi wenyewe na kusaidia katika kuwatambua wanafunzi wengine ambao hawahudhurii skuli.

# Kitini 1.3b: Muhutasari kuhusu maana ya kamati ya elimu mjumuisho ya skuli

## Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli

- huwaleta pamoja wadau wa elimu au walio karibu na skuli na **wenye lengo linalowaunganisha** – kuifanya skuli yao iwe jumuishi.
- ina wawakilishi tofauti **wanaofanya kazi kwa kujitolea.**
- **ipo kwa ajili ya kuwasaidia** walimu, wafanyakazi wengine, wanafunzi na wazazi/walezi – sio kuongeza ngazi nyengine ya urasimu au mzigo. Iwapo kamati itageuka mzigo au kufanya kazi kama chombo chenye urasimu, itakua inakwenda kinyume na kusudio.
- inapaswa kuwa mfano wa maana halisi ya ujumuishi, **na kutoa msaada kiutekelezaji na ushauri** ili wengine waigeuze elimu ya nadharia ya ujumuishi kuwa uhalisia;
- inashughulika na **changamoto zote za ujumuishi wa skuli** ambazo zinaweza kujitokeza katika nyakati tofauti katika kipindi cha mwaka wa masomo – kwa mfano, sababu na suluhisho kwa matokeo ya fujo dhidi ya wanafunzi wengine, utoro au uchelewaji – mambo ambayo ni kikwazo kwa ujumuishi.

# Kitini 1.4a: Simulizi ya Yussuf – muhutasari

Yussuf alizaliwa akiwa haoni. Anaweza kuona mwangaza hafifu tu, lakini hawezi kuona chochote chengine. Hata hivyo, anapenda sana kujituma. Anacheza na ndugu zake na majirani na amekua akijifunza kumsaidia mama yake na baba yake baadhi ya majukumu ya nyumbani. Ana umri wa miaka minne na wazazi wake wanatamani aanze skuli katika umri sawa na watoto wengine, atakapotimiza miaka sita. Wanafahamu kwamba wanapaswa kujipanga sasa kwa kuwa jambo hilo halitokua rahisi.

Skuli iliyopo jirani na anapoishi haipo tayari kumsajili/kumdahili Yussuf. Wanadhani angepaswa kumuandikisha katika skuli maalumu. Lakini skuli ya karibu ipo kilomita 240 kutoka anapoishi, na ina uwezo wa kuandikisha wanafunzi wachache tu kila mwaka. Safari ya kwenda huko ni ndefu na ina gharama kubwa kiasi kwamba, Yussuf atalazimika kuonana na familia yake mara mbili tu kwa mwaka. Alihuzunika sana aliposikia hivi na akasema kwamba hataki kabisa kuandikishwa katika skuli hiyo. Wazazi wake wanakubaliana kwamba ni muhimu Yussuf atumie umri wake wa utoto akiwa na familia na rafiki zake, kwa hivyo wanajitahidi kutafuta ruhusa ya Yussuf kuandikishwa katika skuli jirani.

Skuli inasema kwamba kuna sababu nyingi za kumfanya Yussuf asiweze kuandikishwa katika skuli hiyo. Kwa mfano:

- Skuli haina mwalimu maalumu kwa ajili ya watoto wasioona.
- Walimu wengine hawana uzoefu wa kuwashughulikia watoto wenye ulemavu. Wana hofu.
- Mwalimu mwengine ana wasiwasi kwamba watoto wengine watamnyanyasa Yussuf.
- Afisa elimu wa Kijiji anasema kwamba ni sera ya serikali kwamba watoto wasioona wanapaswa kuandikishwa katika skuli maalumu.
- Mwalimu Mkuu anasema kwamba skuli haina fedha za kununulia vitabu vya nukta nundu au vifaa vya kuandikia.
- Walimu wanahisi kwamba skuli yao ina mazingira hatari mno kwa mtoto mwenye ulemavu kwa sababu ya ngazi nyingi na mashimo.

Wazazi wa Yussuf waliemewa na orodha ndefu ya sababu za kumfanya mtoto wao asiandikishwe katika skuli hiyo. Wakahisi hakuna namna zaidi ya kumuandikisha katika skuli maalumu – ndio nafasi pekee kwa Yussuf kusoma.

Siku moja mama yake alikua anauza mboga sokoni alipokutana na mteja mpya aliyekuja kununua tungule. Alikua haoni lakini mama yake Yussuf alishangazwa na jinsi alivyoweza kwa haraka na usahihi kuhesabu pesa bila ya kuziona. “Natumai mwanangu ipo siku nae ataweza kuhesabu pesa kama unavyoweza wewe”. Hapa ilikua ndio mwanzo wa mazungumzo. Yule mwanamke asiyeona, Edith, alikua ni mwanachama wa jumuiya ya watu wenye ulemavu, na alisema anaweza kuwapa ushauri wazazi wa Yussuf. Walikubaliana wakutane siku iliyofuata.

**Miaka miwili baadae Yussuf aliandikishwa katika skuli ya kijijini kwao. Ni vipi hili lilitokea?**

# Kitini 1.4b: Simulizi kamili ya Yussuf

Yussuf alizaliwa akiwa haoni. Anaweza kuona mwangaza hafifu tu, lakini hawezi kuona chochote chengine. Hata hivyo, anapenda sana kujituma. Anacheza na ndugu zake na majirani na amekua akijifunza kumsaidia mama yake na baba yake baadhi ya majukumu ya nyumbani. Ana umri wa miaka minne na wazazi wake wanatamani aanze skuli katika umri sawa na watoto wengine, atakapotimiza miaka sita. Wanafahamu kwamba wanapaswa kujipanga sasa kwa kuwa jambo hilo halitokua rahisi.

Skuli iliyopo jirani na anapoishi haipo tayari kumsajili/kumdahili Yussuf. Wanadhani angepaswa kumuandikisha katika skuli maalumu. Lakini skuli ya karibu ipo kilomita 240 kutoka anapoishi, na ina uwezo wa kuandikisha wanafunzi wachache tu kila mwaka. Safari ya kwenda huko ni ndefu na ina gharama kubwa kiasi kwamba Yussuf atalazimika kuonana na familia yake mara mbili tu kwa mwaka. Alihuzunika sana aliposikia hivi na akasema kwamba hataki kabisa kuandikishwa katika skuli hiyo. Wazazi wake wanakubaliana kwamba ni muhimu Yussuf atumie umri wake wa utoto akiwa na familia na rafiki zake, kwa hivyo wanajitahidi kutafuta ruhusa ya Yussuf kuandikishwa katika skuli jirani.

Skuli inasema kwamba kuna sababu nyingi za kumfanya Yussuf asiweze kuandikishwa katika skuli hiyo. Kwa mfano:

- Skuli haina mwalimu maalumu kwa ajili ya watoto wasioona.
- Walimu wengine hawana uzoefu wa kuwashughulikia watoto wenye ulemavu. Wana hofu.
- Mwalimu mwengine ana wasiwasi kwamba watoto wengine watamnyanyasa Yussuf.
- Afisa elimu wa Kijiji anasema kwamba ni sera ya serikali kwamba watoto wasioona wanapaswa kuandikishwa katika skuli maalumu.
- Mwalimu Mkuu anasema kwamba skuli haina fedha za kununulia vitabu vya nukta nundu au vifaa vya kuandikia.
- Walimu wanahisi kwamba skuli yao ina mazingira hatari mno kwa mtoto mwenye ulemavu kwa sababu ya ngazi nyingi na mashimo.

Wazazi wa Yussuf waliemewa na orodha ndefu ya sababu za kumfanya mtoto wao asiandikishwe katika skuli hiyo. Wakahisi hakuna namna zaidi ya kumuandikisha katika skuli maalumu – ndio nafasi pekee kwa Yussuf kusoma.

Siku moja mama yake alikua anauza mboga sokoni alipokutana na mteja mpya aliyekuja kununua tungule. Alikua haoni lakini mama yake Yussuf alishangazwa na jinsi alivyoweza kwa haraka na usahihi kuhesabu pesa bila ya kuziona. “Natumai mwanangu ipo siku nae ataweza kuhesabu pesa kama unavyoweza wewe”. Hapa ilikua ndio mwanzo wa mazungumzo. Yule mwanamke asiyeona, Edith, alikuwa ni mwanachama wa jumuiya ya watu wenye ulemavu, na alisema anaweza kuwapa ushauri wazazi wa Yussuf. Walikubaliana wakutane siku iliyofuata.

**Miaka miwili baadae Yussuf aliandikishwa katika skuli ya kijijini kwao. Hili lilitokeaje?**

Edith kwanza aliwasaidia wazazi wa Yussuf kukutana na afisa elimu wa wilaya (DEO). Alikuwa mkali, na wazazi wa Yussuf walishaomba kukutana nae mara 3 bila ya mafanikio. Edith alitumia uhusiano alionao na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu kushinikiza kufanyika kikao cha saa moja. Katika kikao hicho alihadithia uzoefu aliopitia katika maisha yake ya kutafuta elimu (katika mazingira yote, ya skuli maalumu na jumuishi), na alieleza juu ya mikataba ya kimataifa inayosisitiza mifumo ya elimu iwe jumuishi. Hatimae, afisa elimu wilaya alikubali kwamba Yussuf aandikishwe katika skuli jirani na anapoishi, iwapo Edith ataisaidia skuli kutatua orodha ndefu ya changamoto zilizotajwa. Pia alikubali kuwasilisha ajenda ya kujadili mabadiliko ya sera ya elimu atakapohudhuria kikao kijacho katika Wizara ya Elimu.

Hatua nyengine aliyochukua Edith ilikuwa ni kuwashawishi baadhi ya walimu kutembelea nyumbani kwao Yussuf, kumuangalia Yussuf akicheza na kusaidia kazi za nyumbani. Walipofika, mwalimu mmoja aliuliza “yuko wapi mtoto asiyeona?” walitarajia kumkuta Yussuf akiwa ametulia, bila ya kukimbia akicheza mpira! Baada ya kujionea yote haya walimu wote walikubaliana kwamba Yussuf hakuwa ‘asiye na maana’ kama walivyotarajia, lakini bado walikuwa na hofu ya kumfundisha.

Edith na wenzake katika Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu walishirikiana kwa miezi kadhaa kutafuta jumuiya ambayo ingewapatia baadhi ya walimu mafunzo. Walimu walipatiwa wiki moja ya mfunzo mara tatu katika vipindi tofauti vya likizo. Mafunzo yalijumuisha masuala ya ulemavu na kutumia mbinu za kufundishia zinazomlenga mwanafunzi, na mafunzo hayo yalitolewa na wakufunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu. Walimaliza mafunzo yao miezi 6 kabla ya kuandikishwa kwa Yussuf. Ulipofika muda wa Yussuf kuanza

skuli, walimu walimwambia Edith kwamba walikuwa wanajisikia wanawafundisha watoto wote vizuri zaidi kuliko hapo kabla, kwa hivyo walikuwa wapo tayari kumpokea Yussuf. Yussuf alipoandikishwa, mwalimu wake wa darasa alishirikiana na Edith, Yussuf pamoja na wazazi wake kuandaa orodha ya shabaha zao za awali. Hii ilijumuisha vitu ambavyo Yussuf aanze kujifunza, jinsi gani mwalimu atamsaidia, na usaidizi gani wa ziada ambao mwalimu atauhitaji kutoka kwa wenzake, Edith, wazazi au watu wengine.

Skuli ilikua haina uwezo wa kumuajiri mwalimu mtaalamu wa elimu maalumu, na wazazi wake Yussuf walikua na hofu kwamba nani angeweza kumfundisha mtoto wao ujuzi kama vile wa kusoma nukta nundu na kuandika. Baada ya utafiti wa muda, Edith aliwaalika vijana wawili wasioona kutoka katika Kijiji chengine, kumtembelea Yussuf mara mbili kwa wiki, ili kumfundisha misingi ya kusoma na kuandika nukta nundu. Vijana hawa walikuwa wamemaliza mafunzo katika skuli maalumu lakini walikuwa hawajaajiriwa. Walikua tayari kujitolea iwapo mama yake Yussuf angewapatia chakula cha mchana. Mmoja kati ya vijana hawa aliweza kuishawishi skuli aliyosoma kuchangia ubao wa nukta nundu na kalamu ya kuandikia nukta nundu kwa ajili ya Yussuf. Kijana mwengine wa kujitolea alifurahia sana kumsaidia Yussuf kiasi kwamba – kwa msaada wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu – alitunukiwa udhamini wa masomo ya kwenda kusomea ualimu, mwaka unaofuata. Anakusudia kufanya mafunzo yake ya vitendo katika skuli anayosoma Yussuf akitumai siku moja awe muajiriwa kamili wa skuli hiyo.

Walimu waliamua kuwaandaa watoto wengine kumpokea Yussuf skuli, kwa hivyo waliandaa shughuli mbalimbali kuwafundisha watoto kuhusu ulemavu na haki za watoto. Watoto walifahamu haraka sana na wakaanza kuuliza iwapo wangeweza kufanya maboresho yoyote kuifanya skuli iwe salama kwa Yussuf atakapowasili. Walitumia muda wao wa mapumziko kuokota mawe kujaza katika uwanja wa kuchezea ili uwe tambarare na salama. Pia walitumia mawe kuweka alama za njia kutoka getini kuelekea darasani na maktaba. Watatu kati yao walikubaliana kumuonesha Yussuf njia hizi siku ya mwanzo atakapowasili. Baadhi ya watoto walikwenda kuzungumza na wazazi wao nyumba

# Kitini 1.4c: Mkabala wa mbinu pacha

Elimu mjumuisho ina lengo la kubadilisha mfumo, na sio kumbadilisha mwanafunzi. Lakini kuzingatia mabadiliko ya mfumo haimaanishi kwamba tunapaswa kupuuza mahitaji **maalum** ya kujifunza ya mwanafunzi **binafsi.** Tunahitaji kukabiliana na kutengwa katika elimu kutoka pande mbili - kwa kukuza mabadiliko ya kimfumo **na** kwa kutoa usaidizi mahususi kwa mahitaji ya kujifunza ya mwanafunzi binafsi. Huu ndio mkabala wa **mbinu pacha**:

**Inazingatia mfumo:**
Kuhakikisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, mitazamo na mbinu zinashughulika utofauti na kukuza ujumuishi. Kuondoa vikwazo.

**Inazingatia mwanafunzi:**
Kuheshimu maoni yao na kutoa msaada unaofaa kwao kama ni haki yao. Hii inasababisha kuwawezesha kupitia uwepo, ushiriki na ufaulu.

Elimu mjunuisho =
Kushughulikia utofauti

# Kielelezo 3.2a: Kuhaulisha mahusiano ya madaraka/madaraka




[Ufafanuzi wa picha: Wanawake wawili wamesimama wanazungumza, wakiashiria kwa mikono. Nyuma yao kuna majengo na bango linalosomeka ‘skuli’. Mwanamke aliyesimama kushoto amevaa mavazi yake yaleyale ya kila siku, na ameinama kidogo kwa mbele huku akiwa amenyoosha mikono na anaonekana mwenye huzuni. Kando yake kuna mtoto mdogo wa kiume aliyevaa fulana rangi ya njano na miwani myeusi akiwa ameshika fimbo ndefu. Mwanamke anaezungumza nae amevaa kwa umaridadi mkono wake mmoja akiwa ameshikilia kiuno. Anaonekana amekasirika au mkali akimjibu yule mwanamke mwengine].



[Ufafanuzi wa picha: Kuna watu 9 waliokaa katika umbo la nusu duara katika mabenchi katika chumba chenye madirisha matatu nyuma. Kupitia kwenye madirisha unaona majengo ambayo yanafanana na skuli. Miongoni mwa waliokuwepo katika kikundi ni mwanamme aliyekaa kwenye kitimwendo, mzee mmoja akiwa ameshika fimbo ya kutembelea na mtoto wa kike aliyevaa sare za skuli akiwa na mguu mmoja na gongo la kutembelea, na wanawake wengine watatu na mwanamme mmoja. Mwanamke yuleyule ambae huvaa nguo zile zile kila siku nae pia yupo katika kikao anazungumza. Kando yake, aliyekaa kwenye benchi ni mtoto mdogo wa kiumealiyevaa miwani myeusi akiwa ameshika fimbo ndefu. Watu wote wanamsikiliza yule mwanamke na nyuso zao zinaonesha kuguswa mno**].**




[Ufafanuzi wa picha: Kuna kundi kubwa la watu 20 au 30 wakiwa wamekusanyika  kwenye viti, nje ya skuli. Mwanamke aliyevaa mavazi ya kila siku amesimama akiuhutubia mkusanyiko. Kando yake kuna mwanamme aliyesimama akiwa amevaa shati na suruali, akiwa ameshika mkono wa mtoto yule yule aliyevaa sare za skuli huku ameshika fimbo ndefu. Watu waliokaa kwenye viti wanamsikiliza kwa umakini mwanamke anayezungumza. Miongoni mwao, aliyekaa mstari wa mbele, ni mwanamke mtanashati, anayesikiliza. Anaonekana mwenye kukubaliana na kinachozungumzwa. Pia kuna watu wengine ambao si wapya kama vile mwanamme aliyekaa kwenye kitimwendo, mzee mwenye fimbo ya kutembelea (mkongojo), mwanamke aliyevaa hijabu na mtoto wa kike mwenye mguu mmoja].

# Kitini 3.2b: Kufahamu mahusiano ya kimadaraka/madaraka

Kuna vyanzo tofauti vya madaraka au sababu katika maisha zinazowawezesha watu kuwa na madaraka, ambapo sisi kama mtu mmoja mmoja hupata madaraka hii kwa kujua au kutokujua. Kwa mfano:

- Elimu, uzoefu wa kazi, hadhi na mali
- kipaji cha kusikiliza, nafasi katika mamlaka, madaraka ya ushawishi
- kipaji cha uchambuzi, udhibiti juu ya rasilimali, ujuzi wa utatuzi wa migogoro

Madaraka yanaweza kuwa ya mtu binafsi au ya kikundi cha watu, kama inavyooneshwa na tafsiri ifuatayo:

> **“Madaraka ni uwezo wa kutekeleza malengo binafsi na kuwashawishi wengine kufikia malengo hayo. Ni uwezo wa kupata tunachokitaka, kuhodhi tulichonacho, na kusawiri matukio katika namna tunayotaka yawe.”**
>
> **“Kwa ngazi ya kikundi, madaraka ni uwezo wa kuunganisha vyanzo tofauti vya madaraka ya mtu mmoja mmoja ili kuleta mabadiliko tunayoyatamani ambyo hunufaisha kikundi badala ya mtu mmoja mmoja.”**

Madaraka yanaweza kugawiwa katika makundi manne:

**Madaraka zaidi:** falsafa hii inaamini kwamba madaraka ni kitu maalumu – mtu mmoja ama kikundi kinapopata madaraka zaidi, wengine hupunguziwa.

**Madaraka kwa:** aina hii ya madaraka yanaelezea aina fulani ya **uwezeshaji.** Inamuwezesha mtu kudhibiti au kusimamia hali fulani kwa manufaa yake.

**Madaraka na:** hii inajumuisha **madaraka ya pamoja** na huonekana pale kikundi kinapotatua changamoto pamoja, na kutengeneza madaraka ambayo ni makubwa kuliko jumla ya madaraka ya watu wanaounda kikundi hicho.

**Madaraka ndani ya:** madaraka haya yanaishi ndani ya mtu na yanawakilisha madaraka ya ndani. Inatokana na **kujikubali na kujiheshimu,** ambayo nayo hutokana na kuwaheshimu wengine na kukubali kwamba watu wote ni sawa.

- 'Madaraka dhidi/ zaidi' ni mtazamo ambao mara nyingi tunautumia kuonea madaraka.
- Tunachukulia kwamba iwapo mtu mmoja/kikundi katika uwiano ana madaraka zaidi, waliobaki katika uwiano huo lazima wawe hawana madaraka. Tunachukulia kwamba iwapo asiye na madaraka (dhaifu) atapata madaraka mpya, aliye na madaraka zaidi lazima apoteze sehemu ya madaraka zake, kwa sababu kuna kiwango kidogo sana cha madaraka ambazo watu wanaweza kushirikiana pamoja!
- Hii inaonekana katika mijadala ya jinsia, ambapo wanaume huhofia mwanamke kuwa na madaraka zaidi kwa sababu ya athari hasi ambayo wanadhani itawakumba. Jamii inaamini kwamba usawa wa jinsia unamaanisha kwamba wanaume watalazimika kusalimisha sehemu ya madaraka yao kwa wanawake na kwa kufanya hivyo wanaume watapoteza nafasi na hadhi yao.
- Mtazamo huu wa uwiano wa madaraka ambapo upande mmoja unaweza tu kupata madaraka iwapo upande mwengine utapoteza hautotusaidia sisi kufikia lengo la jamii jumuishi na isiyo na ubaguzi.
- Kufikia malengo yetu tunahitaji kubadilisha namna ambavyo sisi (na wengine) tunavyoifahamu madaraka. Hii inamaanisha kutafuta namna ya kurahisisha katika kazi zetu uwepo wa 'madaraka ndani ya' na 'madaraka kwa' – na kuifahamu zaidi madaraka kama rasilimali isiyo na mipaka – bali kuna madaraka ya kumtosheleza kila mtu!

Imetokana na matini yaliyoma katika: Lewis, I (2005) *Making a Difference: Training materials to promote diversity and tackle discrimination*, Save the Children

# Kielelezo 5.2: Nakala ya video: Bibi Marvellous Mubi, akitafakari jukumu lake kama Mratibu wa Elimu Mjumuisho, Skuli ya Shungu, Zambia

Jina langu ni Marvellous Mubi, ninatoka skuli ya msingi na sekondari ya Shungu. Mimi ni Mratibu wa Elimu Mjumuisho wa Skuli. Kazi zangu nyingi ninazofanya kama Mratibu wa Elimu Mjumuisho kwanza ni kuratibu programu za elimu mjumuisho na pia kupanga shughuli hizi, kama unavyojua ni skuli kubwa ambayo inahusisha kazi nyingi. Skuli yetu ni kuanzia darasa la kwanza hadi darasa la kumi na mbili, ikimaanisha kwamba wanafunzi hawa wote wanatakiwa kushirikishwa katika elimu hii mjumuisho. Kwa hivyo kuna haja ya mimi kupanga shughuli zao kisha pia kutekeleza [sauti haisikiki] mipango tunayofanya kama walimu kama uongozi, kama skuli tunavyotekeleza katika programu yetu. Kisha jukumu jengine ninalofanya ni, jukumu langu jengine ni kuanzisha Kitengo cha Usaidizi wa Kujifunza, sio tu kukianzisha bali pia [ku]simamia shughuli zinazofanyika katika kitengo hicho. Kitengo cha Usaidizi wa Kujifunza ni chumba ambamo kama kama mratibu wa elimu mjumuish, ninaendesha shughuli zake. Hiki ni chumba ambacho shughuli za elimu mjumuisho hufanywa kama vile tunapozungumzia utengenezaji na urekebishaji wa vifaa mbalimbali, hiki ni chumba ambacho walimu huwa wanakaa na kuandaa rasilimali na nyenzo mbalimbali, ambazo zinatumiwa na wanafunzi na walimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani.

Kisha pia ninasaidia mahitaji binafsi ya mtoto, kwa mfano kama kuna mtoto ana mahitaji ya kielimu kama vile mtoto anayejifunza polepole; Ninamsaidia mwalimu wa mwanafunzi huyo katika chumba hiki cha usaidizi wa kujifunza na pia nitakutana na mtoto huyu kwa msaada wa mwanafunzi mmoja mmoja. Tunazungumzia elimu mjumuisho ambapo kila mtu anahitaji kushiriki na kila mtu anahitaji kufikia kitu fulani. Na pia hiki ndicho chumba ambacho tunakutana na wazazi au walezi wa watoto hawa tunaowafundisha. Tunapozungumzia elimu mjumuisho, tunazungumzia kuhusisha kila mtu, ambaye ni mdau katika elimu ya mtoto huyu. Kwa hivyo, wazazi ni muhimu sana tunapotaka kubaini tatizo la mtoto, hivo tunawaita na hawa wazazi waje katika Kitengo cha usaidizi wa Kujifunza ambako wanakaa na mwalimu na kujadili tatizo la mtoto au wakati mwengine ni kuwatia moyo wazazi tu au kuwapa ushauri wa jinsi ya kumsaidia mtoto huyo.

Halafu pia jambo jengine ni kufanya mikutano tu na walimu, sio kila kitu tunachokijua, tunakaa, tunapanga tunasaidiana jinsi ya kushughulikia

wanafunzi wneye mahitaji maalum ya kielimu, wanaojifunzama polepole, wanaohitaji kazi tofauti kidogo au wakati mwengine kama mwalimu nikitaka kufanya kazi ya kurekebisha/ kubadilisha kitu naomba ushauri kwa wenzangu kuhusu namna ambavyo nitamsaidia mtoto ambaye ana tatizo kama hili.

Kisha pia labda jukumu jengine la Kitengo cha Usaidizi wa Kujifunza ni kusaidia pia katika kutengeneza mipango ya elimu ya mtu binafsi, ikiwa mtoto ana shida kwa mfano, mwalimu anayemfundisha mtoto huyo anapaswa kuwa na uwezo wa kupanga mpango wa kujifunza kwa mtoto huyu na hapa ndipo suala la Mpango Binafsi wa Kuijifunza (IEP) huwa muhimu .Katika mipango ya mtu binafsi ya elimu kama mwalimu au timu tunashirikiana na walimu wengine, kukaa chini, kujadili kisha kupanga jinsi tunavyoweza kumsaidia mtoto huyu au mwanafunzi anayehitaji msaada, katika kazi yake ya kitaaluma.

# Kitini 5.3: Shughuli anazoweza kushiriki mratibu wa elimu mjumuisho wa skuli

## Skuli

- Kuujengea uwezo na kuuhamasisha uongozi wa skuli, walimu na wafanyakazi wengine;
- Kuhakikisha kwamba mipango ya skuli ni jumuishi;
- Kutathmini miundombinu kuona iwapo inakidhi vigezo vya ufikiwaji;
- Ushauri juu ya kutengeneza aina fulani ya vitendea kazi;
- Mafunzo kuhusu mbinu jumuishi katika darasa ;
- Kuimarisha ushirikiano baina ya skuli na jamii;
- Kuwafuatilia na kuwatathmini wanafunzi mmoja mmoja;
- Kuandaa mijadala ya vikundi kwa walimu na wanafunzi;
- Kupendekeza shughuli kwa mkabala wa ujumuishaji wa skuli nzima.

## Kwenye jamii

- Kukuza uelewa katika ngazi ya jamii;
- Kujenga ushirikiano baina ya skuli na jamii;
- Kutembelea mwanafunzi mmoja mmoja nyumbani kwao inapobidi;
- Kuhudhuria vikao vya Kijiji;
- Kuandaa rufaa kwa huduma zinazopatikana kijijini – kwa mfano, huduma za uchunguzi wa
- Kubaini ujuzi na vifaa vinavyopatikana kijijini ambavyo vinaweza kutumika skuli – kwa ajili ya kufundishia, n.k.
- Kuwafundisha watendaji wa kujitolea wa Kijiji mbinu za kuwabaini wanafunzi;
- Kuandaa mafunzo ya mtaalamu kwa ajili ya wazazi/walezi yatakapohitajika.

## Na wizara ya elimu na Michezo/ katika ngazi ya sera

- Kuhudhuria vikao vya baraza kwa lengo la kukuza uelewa na kuhoji kuhusu fursa za ufadhili;
- Kukuza uelewa kupitia vyomba vya habari – redio ya kijiji na magazeti;
- Kuhudhuria vikao vya mipango ili kuhakikisha kwamba mipango yote ni jumuishi;
- Kuzihusisha Jumuiya zisizo za Kiserikali na asasi za kijamii katika mafunzo yoyote kuhusu elimu jumuishi katika vituo vya elimu au maeneo mengine muafaka.

# Kielelezo 6.1: Picha za jamii



[Ufafanuzi wa picha: [Ufafanuzi wa picha: Kuna kijana anayeonekana katikati ya picha. Kando yake kuna punda wawili na yeye ameinama na kushikilia mguu mmoja wa mbele wa mmoja kati ya punda hao. Nyuma ya kijana huyo kuna punda mwengine ambaye amefungwa kwenye mkokoteni wenye magurudumu mawili. Kuna pipa la bluu lililofungwa kwenye mkokoteni. Pia kunaonekana katika picha hii  mwanamke ambaye anatembea karibu na mkokoteni. Nyuma ya picha kuna jengo dogo lililoharibika. Haijulikani jengo hilo ni nini, lakini kwenye moja ya kuta zake, kumeandikwa maneno "Imefadhiliwa na Tume ya Ulaya". Mbele ya jengo hilo kumeegeshwa gari kubwa jeupe. Eneo la mbele ya jengo ambalo kijana ameinama na mwanamke anatembea, kuna mchanga mkavu, mgumu na mawe mengi juu yake. Pia kuna takataka nyingi chini, hasa chupa za plastiki na vifungashio mbalimbali]'



[Ufafanuzi wa picha: Katika picha hii kuna kibanda kikubwa kilichotengenezwa kwa vipande vya mabati ambavyo vimeunganishwa. Kuna michoro ya picha katika baadhi ya sehemu za kibanda. Kuna mtu mmoja ameketi kwenye sanduku jeupe la plastiki, nje kidogo ya kibanda hicho. Karibu na mtu huyo kuna dumu kubwa kubebea maji lenye rangi ya njano. Kuna takataka nyingi - mirija ya plastiki, mifuko mikubwa myeupe iliyorundikana, makopo matupu na pia kuna kitu kinachoonekana kuwa ni godoro bovu na chafu sana. Nyuma ya kibanda hicho kuna rundo kubwa la takataka. Kuna mtu amesimama kwenye rundo la takataka akilitazama na kuna mtu mwengine amesimama akitazama rundo hilo la takataka. Kwa nyuma pia kuna gari kubwa karibu na jaa].




[Ufafanuzi wa picha: Katika picha hii kuna kibanda kikubwa kilichotengenezwa kwa vipande vya mabati ambavyo vimeunganishwa. Kuna michoro ya picha katika baadhi ya sehemu za kibanda . Kuna mtu mmoja ameketi kwenye sanduku jeupe la plastiki, nje kidogo ya kibanda hicho. Karibu na mtu huyo kuna dumu kubwa kubebea maji lenye rangi ya njano. Kuna takataka nyingi - mirija ya plastiki, mifuko mikubwa myeupe iliyorundikana, makopo matupu na pia kuna kitu kinachoonekana kuwa ni godoro bovu na chafu sana. Nyuma ya kibanda hicho kuna rundo kubwa la takataka. Kuna mtu amesimama kwenye rundo la takataka akilitazama na kuna mtu mwengine amesimama akitazama rundo hilo la takataka. Kwa nyuma pia kuna gari kubwa karibu na jaa].

## Kielelezo 6.2 Taswira pana ya jamii



[Ufafanuzi wa picha: Picha inaonesha mandhari ya jamii. Upande wa juu wa mkono wa kushoto kwa nyuma kuna msikiti na nje ya msikiti kuna kundi la watu wamesimama pamoja wakizungumza. Mmoja wa watu hao ni Imamu wa msikiti huo. Kanisa liko kwenye miteremko ya kilima na upande wake wa kulia kidogo kuna vijana wa kiume wawili wanaofukuzana. Karibu na wavulana hawa kuna ngamia wawili ambao wanaongozwa na mtoto mwengine mdogo wa kiume. Katika mteremko wa kilima katikati ya picha kwa mbali pia kuna kundi la mahema makubwa ambayo yanaonekana kama kambi ya wakimbizi. Upande wa kulia wa kambi ya wakimbizi na katika kona ya juu ya mkono wa kulia wa picha kuna jengo lenye madirisha mengi na mnara mkubwa wa saa katikati. Nje ya jengo hili kuna alama inayosema "Jaamacad" na mbele ya ishara hiyo ni watu watatu. Vijana wawili wanazungumza na mmoja ana mkoba. Mbele yao kuna mwanamme akitoka nje ya jengo akiwa amebeba folda.

Karibu kidogo upande wa kulia wa picha kuna mwanamme amesimama chini ya kibanda kidogo kilichotengenezwa kwa bati. Chini ya kibanda kuna fremu kumi za kitanda cha mbao zilizopangwa katika safu mbili. Karibu na kibanda hicho kuna mbuzi wawili na watoto wawili wanaotembea. Karibu na kibanda katikati ya picha kuna jengo la saruji. Jengo hilo lina maandishi yanayoonesha kuwa ni kituo cha polisi. Maofisa wa polisi wanawake wawili wamesimama nje ya jengo hilo wakizungumza na afisa mwengine wa kiume wa polisi amesimama nje akilinda lango la kuingilia kituo cha polisi. Unaweza pia kumwona afisa mwengine wa polisi wa kiume akiwa amesimama ndani ya kituo.

Mbele ya kituo cha polisi kuna mtu akielekea kwenye jingo jengine. Jengo analotembea lina milango ambayo iko wazi na ndani ya duka kuna nguo zinazoning'inia ambazo zinauzwa. Kuna mtu yuko dukani ameshika nguo. Katika duka pia kuna mtu ameketi akiwa anashona kwenye meza ndogo.

Upande wa kushoto wa picha mbele kuna kibanda cha mbao na paa la bati. Ndani ya kibanda hicho kuna sufuria mbili zinazochemka. Nje ya kibanda hicho watu wameketi kwenye meza mbili ndogo. Katika meza moja kuna mwanamme mzee na mwanamke kijana wakizungumza, na pana meza ndogo kati yao. Pembeni yao kuna kijana ameketi peke yake kwenye meza na ana sahani ya chakula mbele yake juu ya meza.

Mbele kabisa ya picha ni *Bajaji,* dereva na abiria.

Katika upande wa mbele wa kulia wa picha kuna kibanda kirefu chenye paa la bati. Mbele ya kibanda hicho kuna baadhi ya wanawake wamekaa kwenye viti vidogo na mbele yao kuna mbogamboga ziliwekwa juu ya kitambaa kilichotandikwa chini. Kuna mwaname na mwanamke wananunua mbogamboga. Chini ya paa, muuzaji mmoja ameketi na mtoto na muuzaji mwengine ameshika mtoto.

# Kielelezo cha 6.2: Visa vya igizo-dhima

1. Mwanachama wa Shirikisho la Jumuiya za Watu wenye Ulemavu amealikwa kuhudhuria mkutano wa kijiji ili kujadili idadi kubwa ya wanafunzi wasiohudhuria skuli. Mkutano huo umeandaliwa na unaongozwa na Afisa Elimu wa Wilaya ambaye hajui la kufanya kuhusu wanafunzi hao. Waliohudhuria mkutano huo ni pamoja na kikundi cha wanawake wa kijiji hicho, mwalimu mkuu wa skuli iliyo katika eneo hilo, baadhi ya wazazi, wazee wa kijiji na wanajamii. Mwanachama wa Shirikisho anachelewa kufika, hasikilizi na anazungumza kwenye simu yake ya mkononi wakati wa mkutano ukiendelea. Hachukui maelezo. Hazungumzi na mtu yeyote wala haombi kukutana na wanafunzi.

2. Kikundi kipya cha wazazi wa watoto wenye ulemavu kimeanzishwa katika jamii. Katika mkutano wao wa kwanza wanamwomba mwanachama wa Shirikisho kuja na kuwaeleza kuhusu elimu mjumuisho. Mwanzoni mwa mkutano mwanachama wa Shirikisho anaweza kuona kwamba wazazi wana wasiwasi sana na aibu. Mwanachama wa Shirikisho anajaribu kuwaomba wamweleze kuhusu mtoto wao na kwa nini waliamua kujiunga na kikundi hiki. Mwanachama wa Shirikisho anapoorodhesha kwa heshima hadithi zao, hutumia uzoefu walioshiriki kueleza elimu mjumuisho ni nini na jinsi ilivyo muhimu kwa mtoto wao. Baadhi ya wazazi hawana uhakika kabisa kuhusu baadhi ya mambo ambayo amesema na anamwuliza maswali magumu. Kabla ya kujibu anawauliza wazazi wengine kama kuna yeyote ambaye angependa kujaribu kujibu swali hilo ili wote wajifunze kutoka kwa kila mmoja wao.

3. Bibi mmoja anamkabili mwanachama wa Shirikisho wa eneo hilo. Anahuzunika na kulia kwa sababu wajukuu zake wawili 'watukutu' wanaendelea kutoroka skuli na kupata matatizo. Mwanachama huyo wa Shirikisho hana subira na hana muda wa kuzungumza naye. Anamuuliza babu na bibi kama wajukuu zake ni wana ulemavu - wanasema hapana. Mwanachama wa Shirikisho anamfukuza bibi huyo na kusema kwamba hawezi kusaidia kwa sababu yeye anashughulikia masuala yanayohusu ulemavu tu. Anaonekana ni mkali na hana makabala mzuri wa kuzungumza na watu. Pia hamwelekezi bibi huyo kwa mtu mwengine yeyote ambaye angeweza kumpa msaada na ushauri.

4. Mwenyekiti wa Shirikisho katika eneo fulani anaalikwa kuzungumza kwenye kikao cha Kamati ya Usimamizi wa Elimu ya Wilaya. Jukumu lake ni kuongeza uwelewa juu ya hali ya sasa ilivyo katika skuli za eneo hilo na kutoa maelezo ya kazi ambayo (Kamati za Elimu Mjumuisho za Skuli) SITs zinavyofanya kazi  ili kujenga elimu-jumuishi katika skuli. Wakaguzi wa skuli hawaelewi kikamilifu kuhusu elimu mjumuisho na wanaendelea kuuliza maswali kuhusu skuli maalum. Mwenyekiti anapinga maoni yao na anaingia kwenye mjadala na wakaguzi. Ameghadhibika na anasema kwamba wakaguzi wanarudisha mjadala "nyuma" na kamati inahitaji kusonga mbele.

5. Mwanachama wa Shirikisho pamoja na mwalimu mkuu kutoka skuli fulani, wanatembelea nyumba ya wazazi wa mtoto wa kike ambaye ana ulemavu wa akili. Mtoto huyo ana umri wa miaka 9 na hajawahi kwenda skuli. Wazazi wanamlinda kupita kiasi na hawataki aonewe. Pia wanafikiri kwamba hahitaji kwenda skuli au kuelimishwa kwa sababu ‘hataweza kufanya au kujifunza chochote’. Mwalimu mkuu na mwanachama wa Shirikisho wanaeleza kwa nini mtoto huyo anapaswa kuhudhiria skuli na wanajitahidi kadiri ya uwezo wao kuwashawishi wazazi wa mtoto huyo kumpeleka skuli mtoto wao.  Mwanachama wa Shirikisho anaeleza kwa unyeyekevu jinsi skuli itakavyofanya iwezavyo kuhakikisha kuwa mtoto huyo hanyanyaswi na kwamba atajumuishwa na wenzake wote. Mwanachama wa Shirikisho pia anaelezea kuwa kuna wazazi wengine wenye watoto wenye ulemavu wa akili katika jamii na wameunda kikundi cha wazazi - Anawapa wazazi mawasiliano ya kikundi hicho na kuwashauri wazazi hao wawasiliane na kikundi hicho cha wazazi.